ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo La Kwamtipura.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.

23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.

34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
46.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.

48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
59.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
62.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
63.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
64.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
65.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
66.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
67.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.

68.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
69.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
70.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
71.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
72.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
74.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
75.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
76.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Saba – Tarehe 23 Oktoba, 2009

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 61

Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Daftari la kudumu limeanza uandikishaji katika Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa majimbo mbali mbali, lakini kwa bahati mbaya baadhi ya wananchi wasiolitakia kheri daftari hilo walifanya fujo mbali mbali kwa lengo la kuvuruga mpangilio mzima kwa kupiga watu, kuchoma moto nyumba kumwagia tindi kali (*acid*) Sheha, hayo kwa Pemba na Kaskazini Unguja kisiwani Tumbatu mtu mmoja kapigwa jiwe na kupoteza jicho lake.

(a) Je, Mhe. Waziri vitendo vyote vya fujo vinavyofanywa katika uandikishaji wa daftari unavijua?

(b) Je, Mhe. Waziri hao wote waliofanya vitendo vya kuondoa amani katika zoezi hilo wamechukuliwa hatua gani kisheria?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 61 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, vitendo vyote vya fujo vilivyofanywa katika uandikishwaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ninavijua ambapo baadhi yake nimevishuhudia na baadhi nimepata taarifa zake katika njia tofuati za mawasiliano.

(b) Mhe. Spika, matukio yote na vitendo vyote vya fujo vilivyotokea katika maeneo ya uandikishaji wa Daftari la Wapiga Kura yanaeleweka na wahusika taarifa zao zipo katika vyombo vya sheria

kwa mujibu wa taratibu atakaethibitika na kuingia hatiani sheria itafuata dhidi ya kosa alilolifanya.

Mhe. Haji Faki Shaali: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b)

a) Kwa kuwa msingi mkubwa wa kudumisha na kulinda amani ni kuwepo uhuru, haki na usawa. Haoni kwamba kukosekana mambo haya ndio mara nyingi yanayopelekea kuchafuka amani katika nchi yetu likiwemo zoezi hili la daftari la kudumu.

b) Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakubaliana na kauli ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwamba utii bila ya uhuru ni ujinga, na uhuru bila ya tii ni wendawazimu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: (a) Mhe. Spika, suala la kusema kwamba msingi wa kudumisha uhuru na haki sawa, huu msemo mimi naujua na kimsingi kwa hapa Zanzibar ni kwamba uhuru upo na haki kila mmoja anatendewa haki yake.

b) Mhe. Spika, nashkuru kwa msemo huo wa Mhe. Mwakilishi, mimi naukubali ndio tukasema kwamba kila mmoja anatakiwa awe huru ajiamulie mambo yake yeye mwenyewe. Tatizo linalojitokeza ni kwamba kuna watu wanakuwa hawatumii ule uhuru wao wanatumia utii ndio pale unapotokezea ujinga.Mtu anapolazimishwa agomee kitu fulani wakati anajua ni haki yake ya kimsingi huo ndio ujinga wenyewe na huu ujinga ndio unaoufanya watu wafanye hivyo.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri katika jibu mama amekiri kwamba ziko fujo mbali mbali zimefanyika wakati wa uandikishaji na amesema ziko nyengine ameziona mwenyewe kutoka sehemu mbali mbali.

Kwa kuwa tayari tarehe 26-10-2009 daftari hilo linaingia Mkoa wa Mjini Magharibi ambapo ndio kwenye wasomi wa Chuo Kikuu na linaanzia Wilaya ya Magharibi Shehia ya Mfenesini na Kama. Je, serikali imejiandaa vipi katika kupunguza fujo hizo ambazo tayari maeneo mengine zimeshatokea?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba kuna baadhi ya matukio mimi mwenyewe nimeshuhudia kwa sababu mimi sipendi kufanya kazi ofisini. Mara nyingi katika matukio hupenda niende mwenyewe ili niweze kuona ile hali halisi na tuweze kujua namna gani kuweza kukabiliana nayo. Kwa hivyo, tarehe 26-10-

2009 daftari kweli litaanza katika Wilaya ya Magharibi tumeshajitahidi sana na hivi sasa Jeshi la Polisi wamekuwa wakifanya doria na kuna baadhi ya taarifa za kutaka kufanyika matukio mabaya, hizo taarifa tunazifuatilia kwa karibu tayari kuna baadhi ya watu ambao tuliopata hizo taarifa tunafuatilia taarifa zao.

Kuna matukio kama yatafanyika basi tutaanza kuchukua hatua mara moja kwa sababu kuna taarifa ambazo zile za watu waliohusika katika matukio ya kule Pemba sasa hivi tumo katika kukusanya ushahidi na ndio maana tukasema vyombo vya sheria pale tutakapojiridhisha tutachukua hatua. Kwa hivyo, tunafuatilia na nyenzo za hapa Mkoa wa Mjini Magharibi, mtu yeyote akifanya jambo ambalo ni kinyume cha sheria basi sheria itachukua mkondo wake bila ya kuangalia asili yake, itikadi yake au dini yake.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, katika fujo zilizodaiwa kufanywa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba Mhe. Waziri alinakiliwa na vyombo vya habari akisema kwamba fujo hizo Serikali ya Marekani iko nyuma yake.

Je, alinakiliwa sahihi katika suala hilo na ikiwa ni hivyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mpango gani wa kuona kwamba hali kama hiyo haitokei tena?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kama alivyosema kwamba vyombo vya habari vilininakili vibaya, sikasema fujo zinazotokezea Pemba kama Serikali ya Marekani inahusika. Kwa sababu fujo ambazo zinazotokezea Pemba hakuna Mmarekani hata mmoja aliyeshiriki katika tukio lile au hakuna taarifa hata moja kwamba wao walishiriki katika kupanga huo mpango.

Kwa hivyo, vyombo vya habari na kwa bahati nzuri siku ambayo mwandishi yule aliponihoji alikuwepo na kijana mmoja pale mwandishi wa kimarekani alinisikia wazi wazi jinsi nilivyokuwa nikijibu maswali yale. Kwa hivyo, narejea tena kusema kwamba sijasema kwamba Serikali ya Marekani inahusika na fujo zilizotokea Pemba, isipokuwa wapemba wenyewe ndio waliohusika na fujo ambazo zinatokezea Pemba kwa sababu hakuna mtu mgeni ambaye aliyeshiriki katika zoezi hilo.

Nam. 44

Uuzaji wa Magari ya "*Recondition*"

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:

Takriban katika maeneo mengi ya Mkoa wa Mjini/Magharibi Unguja kumezuka wimbi kubwa la uuzaji wa magari ya "*Recondition*". Imebainika kuwa magari haya hukosa soko kwa kuwa ni mengi sana.

(a) Je, Mhe. Waziri, serikali inakusanya vipi mapato yake kwa wafanyabiashara wa aina hiyo?

(b) Kwa kuwa wafanyabiashara hawa huleta magari ya "*Recondition*". Je, Mhe. Waziri, serikali haioni kuwa itafika wakati Zanzibar itakuwa ni jaa (*dump*) la magari mabovu kama iliyvyo biashara ya mafriji na televisheni?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 44 lenye kifungu a, na b kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali inakusanya mapato yake kutokana na vianzio/nyanja mbali mbali kupitia taasisi zake husika kutoka kwa wafanyabiashara wa aina hiyo.

Kwa mfano:

i. *TRA* inakusanya ushuru wa uingizaji wa magari hayo.

ii. *ZRB* inakusanya kodi ya mapato kwa wafanyabiashara hao.

iii. *MTC* inakusanya ada za uingizaji wa magari.

iv. Shirika la Bandari inakusanya kodi ya upakizi na ushushaji wa mizigo.

v. Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi (KARAKANA) ada ya ukaguzi na upasishaji wa gari hizo.

(b) Mhe. Spika, sheria ya biashara ya magari Nam.7 ya 1985 kiambatisho cha 3 kifungu cha 3 kinamtaka kila anayeleta gari nchini kuleta gari isiyozidi miaka minne tangu kutengenezwa kwake. Aidha,

Halmashauri ya Udhibiti wa Uingizaji wa Magari Nchini iliona ipo haja ya kukaguliwa magari yanayoletwa nchini kule yanakonunuliwa kabla ya kupakiwa. Hata hivyo, Mhe. Spika, maamuzi haya yaliyofanywa mwaka juzi yalikumbana na kutokuabaliana kutoka sekta binafsi. Lakini baada ya kukubaliana, tumekubaliana sasa kwamba magari yawe yanakaguliwa kule yanakotoka.

Hata hivyo, baada ya makubaliano hayo tukajikuta kwamba makampuni mawili tuliyoyachagua kufanya kazi hiyo yameshachukuliwa na wenzetu wa Tanzania Bara na yanawafanyia wao. Kwa hivyo, kwa sasa hivi tuna kazi ya kuingia mikataba na makampuni mengine kwa ajili ya kufanya kazi hiyo. Ni imani yetu kwa hivyo Mhe. Spika, kwamba kwa mtindo huu dhana ya kuifanya Zanzibar kuwa jaa la magari mabovu haitakuwa na nguvu.

Mhe Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri amekiri kwamba yapo magari mengi yanaletwa na wafanyabiashara na hivi sasa tayari wamefanya utaratibu kwamba magari yachunguzwe kila linaloletwa iwe angalau limetengenezwa miaka minne nyuma liweze kuletwa hapa kwa kuuzwa.

Je, mheshimiwa haya ambayo tayari yapo hapa yapo zaidi ya miaka hiyo kuna utaratibu gani unaochukuliwa ?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, kwa yale magari ambayo yako hapa ni imani yetu kwamba yamekidhi viwango vya Halmashauri ya Magari na ndio maana yakaruhusiwa kuingizwa. Kwa hivyo, yale magari ambayo yako hapa hatua za kuchukua ni kuuzwa tu la kama yatachelewa kuuzwa basi mfanyabiashara itabidi aandae mipango yake mwenyewe yakuuza au kusafirisha magari yale.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mimi nakubaliana na Mhe. Waziri kwamba umefika wakati lazima katika nchi yetu tuhakikishe kwamba magari yanayoingia yawe katika hali nzuri ambayo inakubalika kwa usalama wa wananchi wetu wanaotembea mabarabarani. Kwa kuwa Mhe. waziri alijibu kwamba kulikuwa na kampuni mbili ambazo zilikuwa zinafanya uangalizi wa magari kabla ya magari hayo kuja hapa, lakini kwa bahati mbaya kampuni hizo tumetekwa na wenzetu kwa mipango wanayoijua wao.

Je, wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inapata kampuni nyengine za kukagua magari hayo kabla ya kuleta hapa kwetu ili gari hizo ziende sambamba na matakwa ya serikali?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika jibu mama kwamba sasa hivi wizara yangu iko katika mchakato wa kutafuta makampuni mengine mawili ambayo yatafanya kazi hizi. Kwa hivyo, bado tuko katika *process* ya kutafuta hizo kampuni na mara tutakapokubaliana nao basi kazi hii itafanywa mara moja.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a), (b), (c) na (d).

a) Mhe. Spika, hivi sasa katika mji wetu vile vimende vidogo vidogo viko vingi sana na inasemekana vinaletwa kupitia kwenye mafriji na televisheni haya ya mitumba yanayokuja. Je, wizara imechunguza kuna ukweli wowote?

b) Je, vimende hivyo havina madhara kwa wananchi wetu.

c) Marfriji na televisheni hizi zinazokuja wanazifanyia uchunguzi hakuna madawa ya kulevya yanayotiwa humo ndani?

d) Haoni kwamba kuwepo kwa kodi ya uchakavu ndio inayosababisha kuletwa magari mabovu nchini?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, suala la kuwasili kwa mafriji na televisheni na vimende na kufanyiwa uchunguzi ni suala la Shirika la Bandari na wala sio wizara yangu. Suala la kodi ya uchakavu kwamba inaleta watu kuleta vitu vilivyokwisha chakaa sana nchini ni suala la Sera za Kodi na serikali itakaa na kulifikiria.

Nam. 46

Kukosekana kwa Hati za Ukodishwaji wa Ardhi

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:

Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi (*ZIPA*) kwa Pemba inasimamia miradi minane (8) ambayo haijaanza ujenzi na tayari ishapewa vibali tangu 2008. Mamlaka hii imeshindwa kuanza shughuli za ujenzi kutokana na kukosekana kwa Hati za Ukodishwaji wa Ardhi pamoja na kwamba wameshaanza kulipia leseni za Uwekezaji.

(a) Je, Mhe. Waziri suala hili unalijua?

(b) Kwa kuwa wawekezaji huchelewa sana kupata hati ya kukodishwa ardhi, huoni kuwa hiyo itakua ndio miongoni mwa sababu ya kuondoka na kwenda kuekeza nchi za jirani?

(c) Kwa kuwa wizara zote mbili ni za serikali moja (inayotoa leseni na hati ya ukodishwaji wa ardhi) kuna sababu zipi zinazopelekea zoezi hili kukwama?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 46 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi (*ZIPA*) inaelewa kuwa ipo miradi katika Kisiwa cha Pemba ambayo tayari imepata vibali (imeidhinishwa) na *ZIPA*, lakini bado haijaanza shughuli za ujenzi kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo ya kukosekana kwa hati za kukodishwa ardhi (*land lease agreements*) kutoka wizara husika.

(b) Kwa kawaida wawekezaji hawachelewi kupata leseni (inayotolewa na *ZIPA*) kama wamekamilisha masharti yaliyowekwa. Lakini kupatikana kwa leseni au kibali cha *ZIPA* ni hatua moja tu katika utaratibu mzima wa kupata hati ya ukodishwaji ardhi kwa ajili ya mradi husika. Ni kweli kuwa kila mradi unapendelea kukamilisha taratibu zote na kuanza shughuli zake mapema iwezekanavyo. Lakini naamini kuwa kuchelewa kupatikana kwa hati za ukodishwaji ardhi hazikufanywa kwa lengo la kumkomoa mwekezaji, isipokuwa mara nyingi hutokana na haja ya kutimiziwa matakwa ya sheria na taratibu, zikiwemo za kulipa fidia kwa watumiaji wa ardhi waliokutwa katika ardhi hiyo na kuangalia matumizi bora ya ardhi. Baadhi ya wakati ucheleweshaji huo hutokana na matatizo ya wawekezaji wenyewe kutotimiza masharti au taratibu zinazotawala masuala ya aradhi au hata kutovichukua vibali vyao kutoka *ZIPA*.

(c) Kutokana na jawabu yangu ya kifungu (b) iliyotangulia, ni dhahiri kuwa hakuna sababu ya msingi ya kukwama kwa zoezi la kutolewa kwa hati za ukodishwaji ardhi ikiwa ardhi husika haina mgogoro wowote, inafaa kwa aina ya mradi unaoombewa na masharti ya sheria

na taratibu zimefuatwe kwa wakati na pande zote, yaani pamoja na upande wa serikali na wawekezaji wenyewe.

Mhe. Spika, ufafanuzi wa miradi minane iliyokusudiwa hapa ni kama ifuatavyo:-

1.*Pemba Bottlers*	Tayari wanaendelea na kazi.
2.*Pemba Sea Food*	Hawajachukua kibali (*Interim Certificate*) chao kutoka *ZIPA*.
3.*Mkipi Milk Co. Ltd*	Hawajachukua kibali (*Interim Certificate*) chao kutoka *ZIPA*.
4.*Zam Beach Lodge*	Barua ya kuomba *"Land lease"* wameandika karibuni (23/09/2009).
5.*Orion Estate*	Taratibu za Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi zinaendelea.
6.*Pemba Unique Resor*	Mradi umekaa kimya bila ya mawasiliano na *ZIPA* tokea ulipoidhinishwa 2006 licha ya Kupewa onyo la kusitishwa (suspension) kwa ukimya huo.
7.*Elewana Africa Ltd*	Walitaka kisiwa chote cha Kiweni wapewe wao wakati pale walikuta wenzao wameshatangulia. Kwa hivyo, hawajakubaliana na wenzao waliowakuta.
8.*Muyuni*	*Hotel & Spa* Hakuna tatizo lolote, kila kitu kiko sawa.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri amekiri kwamba mpaka hivi sasa iko miradi minane Pemba ambayo tayari imo katika utaratibu wa kutekelezwa. Lakini mheshimiwa tangu juzi hapa tunajadili hii miswada ya sheria ya kuondosha matatizo mbali mbali na moja sheria ya kodi ilikuwa mtu anapita maeneo mengi kuzunguka na imeonekana usumbufu. Sasa imeletwa sheria ya kukusanywa kodi zote kwenye sheria moja ili kuondosha tatizo.

Je, Mhe. Waziri haoni kwamba kibali atoe mwengine, ardhi atoe mwengine haoni kuwa huu ni usumbufu kwa nini haitengenezwi sheria moja ya kuondosha tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, kuna dhana ya *one stop centre* ambayo matakwa ya dhana hii ni kwamba mwekezaji amalize mambo yake yote kwenye kituo kimoja. Lakini kutokana na sheria mbali mbali zinazotawala nchi hasa za ardhi imeonekana kwamba Wizara ya Ardhi bado iendelee kutekeleza sheria ambazo ziko chini ya wizara yake. Kati ya sheria hizo nyengine tulizipitisha hapa juzi tu, kwa hivyo kama waheshimiwa wawakilishi wanaona kuna haja ya sheria ya ardhi kufanyiwa marekebisho na kupewa *ZIPA* hilo sio baya tunaomba wapendekeze.

Hapa naomba nizungumzie mambo mawili kuhusu ardhi. Kuna ardhi ambayo iko chini ya maeneo huru ya uchumi, wawekezaji wa aina huwa hawapati usumbufu wa ardhi kwa sababu mradi ukikubaliwa ardhi inakuwa iko tayari kwa sababu watoaji ardhi hii ni *ZIPA*. Lakini kuna ardhi ambayo inatawaliwa ndani ya sheria za Wizara ya Ardhi. Kwa hivyo, tumetenganisha maeneo mawili ya ardhi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 64

Uchafuzi wa Mazingira

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:

Hivi sasa dunia nzima imekumbwa na hali mbaya ya hewa na baadhi ya maeneo kukumbwa na ukame na hii yote husababisha na uchafuzi wa mazingira kutokana na wingi wa viwanda, ukataji wa miti ovyo bila ya kupanda mingine pia hali inasababisha na theluji/barafu katika vilele vya milima inaendelea kuyayuka kwa nguvu na suala hili karne zote zilizopita halijatokea katika dunia hii.

(a) Je, Mhe. Waziri kwa kuwa na sisi tumo katika dunia wizara ina mikakati gani ya kupunguza tatizo hilo la uchafuzi wa mazingira?

(b) Kwa kuwa mchafuzi mkubwa wa mazingira ni binadamu, Je, kuna taaluma yeyote inayotolewa yenye lengo la kuhami mazingira yetu.

(c) Je, ni maeneo yepi kwa visiwa vyetu yalioathirika zaidi kimazingira?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 64 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, mikakati ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa yanayoikabili dunia hivi sasa kwa lengo la kuondoa au kupunguza athari zinazotokana na mabadiliko hayo katika visiwa vyetu ni pamoja na hii ifuatayo:-

- Kuendelea kutoa elimu ya mazingira juu ya mabadiliko hayo pamoja na athari zake ili kuwahamasisha wananchi wakiwemo viongozi wa ngazi mbali mbali kuachana na matendo yanayosababisha uharibifu wa mazingira na badala yake kuyahifadhi ikiwa ni pamoja na kupanda miti kwa wingi.

- Kuendeleza kushirikiana na vikundi na jumuiya mbali mbali za jamii katika kupanda miti ya aina tofauti kwenye maeneo mbali mbali. Hivyo tunatoa wito kwa wananchi kupanda miti kwa wingi wakati wote.

- Kuandaa mango maalum wa usimamizi wenye uwiyano wa rasilimali za ukanda wa pwani (*Integrated Coastal Management – ICM*) kwa lengo la kuwa na matumizi endelevu yatakayoepusha uharibifu wa mazingira na matumizi ya kupindukia (*over-exploitation*) ya rasilimali hizo. Tayari mikakati imeshaandaliwa na hivi sasa rasimu ya mpango kazi (*Action Plan*) kwa ajili ya utekelezaji wa mikakati hiyo unajadiliwa katika ngazi za wataalamu kabla ya kuthibitishwa na kutangazwa rasmi kwa hatua za utekelezaji.

- Kuendeleza zoezi la kila mwaka la upandaji miti kitaifa katika sehemu mbali mbali za visiwa vyetu, sambamba na kuadhimisha siku ya mazingira duniani ili kuwakumbusha wananchi juu ya mabadiliko hayo.

b) Taaluma juu ya kukabiliana na kujihami na majanga yanayotokana na mabadiliko ya hali ya hewa inatolewa na Idara ya Mazingira kupitia vipindi tofauti kwa kupitia redio na televisheni. Vile vile taasisi za kiserikali kwa ushauri wa Wizara yangu, nazo zimekuwa mstari wa mbele katika kutoa taaluma hiyo juu ya athari za mabadiliko ya hali ya hewa na nini kifanyike ili kukabiliana na hali hiyo visiwani mwetu.

1) Miongoni mwa maeneo yaliyoathirika zaidi ni pamoja na:-

1) Kwa Unguja: Jambiani, Nungwi, Mnemba, Michamvi, Marumbi, Mkokotoni na Bumbwini.

11) Kwa Pemba: Kisiwa Panza, Micheweni Ukele, Tumbe, Kiwani, Kengeja, Kwa Jibwa, Makoongwe, Tibirinzi na Wesha.

Athari hizo zinatofautiana kwenye maeneo ambapo baadhi ya maeneo yanakabiliwa na athari za mmong'onyoko wa fukwe, wakati maeneo mengine yanakabiliwa na tatizo la maji ya bahari kuingia kwenye maeneo ya kilimo na hivyo kuathiri uzalishaji wa mazao ya kilimo na uharibifu wa rasilimali za wananchi.

Mhe. Spika, suala la mazingira ni suala la kitaifa, hivyo kila mmoja wetu ana jukumu la kupiga vita uharibifu huu uliokithiri katika dunia, na Zanzibar ikiwemo katika ramani ya dunia kama aliavyouliza Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba hivi sasa maeneo mengi tayari yameathirika kimazingira na ameyataja kwa Pemba na Unguja. Hivi sasa Kisiwapanza tayari kinaingia maji hasa maeneo ya kilimo.

Je, Wizara kupitia serikali imechukua hatua gani kuhami suala hilo?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwa kweli kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri wangu kwamba tatizo hili tunalijua na kama alivyoeleza kwamba kuna baadhi ya sehemu hizi zina mimong'onyoko kutokana na kuliwa na bahari. Hivi tunavyozungumza Wizara inafanya utafiti wa kina kuhusu maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba pamoja na kufikiria gharama ambazo tutaweza kukabiliana na matatizo hayo zikoje ili hatimaye tukae wizarani kutizama kama ni wizara, na ikiwa hapana budi basi tuweze kuiarifu serikali kuu kwa kushirikiana pamoja katika kutatua au kukabiliana na hali hiyo ya baadhi ya sehemu hizo kuliwa kutokana na bahari.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuzidi kusisitiza, kuelimisha au kuwafahamisha Waheshimiwa Wajumbe kwamba tatizo hili kwa kweli kiasi labda kama wiki tatu au nne kama sikosei nilibahatika kwenda Geneva katika mkutano huu huu ambao unaitwa *Climate Change* au *Global Worming* unaosababishwa na masuala mbali mbali ikiwa pamoja na suala la ukataji miti na kadhalika. Kwa hivyo, imeonekana vile vile kutokana na hali hiyo katika

nchi kwenye sehemu ya *Arctic* , nafikiri wengi tunaifahamu kule ambako kuna mabarafu yanayolingana na milima, ambapo Mhe. Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa alikwenda kule na tukaoneshwa senema yake alipokwenda kufanya ziara kule. Kwa kweli alitoa ripoti yake na ikaoneshwa kwamba mabarafu yale ambayo ni milima yanaanguka kuingia katika bahari, na bahari inakuwa inajaa na kuna uwezekano wa baadhi ya nchi ambazo ziko chini kuweza kuliwa.

Mfano mzuri hivi karibuni kama tumeshuhudia katika televisheni kama sikosei Philippines na nchi nyengine. Na kuna kisiwa fulani nimekisahau nafikiri *Maldaves* watu wameambiwa kule wahamishwe na wamekubali na kuna mipango ya kuhamishwa na kupelekwa katika sehemu nyengine.

Kwa hivyo, nilichokusudia kukisema hapa kua suala la uchafuzi wa mazingira kwa kweli ni *Global,* sio la Zanzibar tu lakini la dunia nzima. Moja katika maazimio yaliyopitishwa pale kwamba dunia nzima watu wote, viongozi wote wa ngazi zote, wafanyabiashara na kadhalika waweze kushirikiana pamoja katika kukabiliana na hali hii.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako nilitaka nitoe tu taarifa hiyo ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Kilimo kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu katujaalia Zanzibar tunaishi katika visiwa, na katika jibu lake Mhe. Waziri amesema kwamba baadhi ya nchi za wezetu hivi sasa kuna visiwa viko karibu ya kufunikwa na bahari au maji mengineyo hata kwenye maziwa. Lakini sisi tunamshukuru Mwenyezi Mungu bado tupo katika usalama huo na tunamuomba atuendeleze katika usalama huo milele na vizazi vyetu.

Je, kwa kuwa nchi yetu imezungukwa na bahari na athari kubwa zinazotokea katika maeneo yetu ni sehemu za fukwe ambazo hazina majabali. Pamoja na juhudi zake hizo Mhe. Waziri amesema kwamba wanafanya mpango wa kulifikisha katika serikali kuu. lakini najua serikali kuu ndio yeye mwenyewe wizara. Wizara ina mpango gani wa makusudi katika maeneo aliyoyataja kama Jambiani Nungwi naongeza na Kiwengwa, Pwanimchangani, Matemwe na kwengineko ambako fukwe zake hazimo katika ule ukanda ambo una majabali au watu wa pwani tunasema makoma.

1) Ana mpango gani wa kuanzisha labda huo utafiti wao wa mwanzo wa kuweka kuta kubwa ambalo litaleta usalama kwa eneo hilo?

2) Katika kuhakikisha kwamba mazingira ya joto duniani, tunatakiwa kupanda miti kwa wingi na kuweka hali nzuri ya kuleta mvua katika

maeneo yetu na kupata usalama wananchi wenyewe, mimea pamoja na wanyama. Wizara kwa kuangalia hili imeweka katika maeneo yanayohifadhiwa kama vile msitu wa Kiwengwa/Pongwe. Msitu huu Mhe. Spika, ukipita barabarani ninamhakikishia Mhe. Waziri ataukuta uko salama, lakini akienda mita 50 tu ndani yake umeliwa na hivi sasa umekuwa kama ni jangwa. Wizara ina mkakati gani wa makusudi kuhakikisha kwamba misitu ya hifadhi inalindwa kwa manufaa ya jamii yetu ili isipotee na kuweka nuru nzuri katika nchi yetu?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nafikiri nimejibu katika maelezo yangu yaliyotangulia kwamba wizara imo katika kufanya utafiti wa kina, imeunda timu ya kuweza kupita maeneo yote haya ambayo yameathirika na yale ambayo yanataka kuathirika ili kujua hali halisi mharibiko ule na kufanya makisio ili kuweza kukabili hali ile. Sasa makisio na mapendekezo yao wataalamu pamoja na wizara yetu itakaa kitako kutizama je, tutafanya vipi katika kukabiliana na hali hiyo?

Kwa mfano, labda tujenge matuta, tujenge kuta na kadhalika. Kwa ufupi kwamba mambo haya yanashughulikiwa na mara tu tukishamaliza huo utafiti basi nafikiri tutachukua juhudi vile vile kuliarifu Baraza lako hatua iliyofikiwa na hatua gani wizara yetu au serikali tunaichukua.

Lakini la pili suala la upandaji wa miti hasa katika misitu ya hifadhi. Mhe. Spika, hili vile vile ni suala ambalo la kila mmoja wetu. Nitatoa mfano wa Korea ambako tumetembelea kule. Mhe. Spika, kule wamepiga hatua kubwa sana katika masuala ya mazingira haya ya upandaji miti. Nini walichofanya? Wamekaa kitako na hakuna uganga waliofanya, uganga mkubwa uliifanywa ni kuamua tu, serikali imeamua na wananchi wameamua kusema basi sasa tulinde mazingira yetu.

Kwa hivyo, kila unapopita Mhe. Spika, vilimani kote kule kama tunavyoona Bara hakuna ruhusa hata mtu kwenda tofauti na hapa kwetu Bara kule utaona misitu katika vilima inachomwa moto, lakini kila unapopita mashamba na mijini watu wanapanda miti mpaka katika nyumba inapandwa miti. Kwa hivyo, ni suala letu sote la kila mmoja wetu kuhifadhi mazingira popote pale alipo.

Mhe. Asha Moh.d Hilal: Mhe. Spika, nashukuru kupata hii nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. ni kweli tunapanda miti lakini hatuishughulikii inakufa, tukishaipanda ndio basi, ng'ombe wanaihujumu pamoja na wanyama wengine. Sasa tuna mpango gani hasa wa makusudi ili kudhibiti hali hii ili miti tunayoipanda ihuwike ili tufanikiwe?

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kama nilivyosema ni tatizo tunarejea pale pale linaturejea sisi na wananchi wetu wenyewe. Hao ng'ombe ni wetu sisi wenyewe Mheshimiwa, maeneo tunayoishi ni yetu sisi wenyewe, jambo kubwa naweza kusema kwamba kila mmoja wetu ashirikiane na wizara yetu na serikali kwanza katika utekelezaji wa sheria zinazohusika na mazingira. Lakini la pili vile vile tushirikiane pamoja katika kulinda mazingira.

SHUGHULI ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya, ya 2009

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Kabla hatujaendelea kuna tangazo moja dogo kwamba Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala itakutana katika ukumbi wa hapo juu hivi sasa. Kwa hivyo, nawaomba Wajumbe wa Kamati wakusanyike hapo kumaliza kazi ya marekebisho ya kanuni.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi ya mwanzo asubuhi hii kuchangia mswada wetu huu ulioko katika mjadala tangu jana. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuandaa mswada ambao umekuja katika wakati muwafaka, baada ya kuona kwamba sheria iliyokuwepo ya madawa ya kulevya bado imekuwa haina meno ya kutosheleza. Kwa hivyo, wameandaa mswada wa sheria mpya ambayo itaweza kuchukua jitihada ya kuweza kulipunguza suala hili au kulimaliza kabisa.

Sasa katika mchango wangu naomba ninukuu katika eneo la madhumuni na sababu halafu nitoe maelezo yangu.

Mhe. Spika, "Mswada huu unasema madhumuni na sababu ya Mswada huu wa Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji haramu wa Madawa ya Kulevya ya Nam. 16 ya 2003 unafutwa na kutungwa sheria mpya ya madawa ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya hapa Zanzibar" Lakini pia katika mswada huo umetiwa kitu muhimu sana kuanzishwa tume ya mawaziri kuratibu usimamizi wa madawa ya kulevya. Moja kati ya malengo makubwa tume hiyo ni kukomesha kabisa biashara ya madawa ya kulevya katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nadhani dhamira ya serikali ni nzuri kwamba hivi sasa imeona pamoja na mswada huu lakini iundwe tume ya baadhi ya mawazidi iweze

kuisimamia na kuiona utekelezaji wake ili mpaka hili suala ambalo hivi sasa limeleta athari kubwa kwa vijana wetu hapa nchini liweze kuondoka kabisa.

Pamoja na hayo vile vile sisi kama viongozi katika jamii nadhani tutakuwa na nafasi kubwa ya kuweza kutoa mchango wetu kupitia kwa mawaziri ama sehemu yoyote ambayo yataweza kufika mawazo yetu na kutekelezwa. Mimi ninachosisitiza hapa kwamba, sheria kutunga ni jambo moja lakini kutekeleza na usimamizi wake ni jambo la pili. Kwa hivyo, naomba sana serikali pamoja na wenzetu hawa waliopendekezwa humu basi jukumu hili walitekeleze. Kwa sababu ile ya mwanzo tuliiona haina nguvu lakini hii tunategemea kwamba kama tutaisimamia vizuri basi tutalipunguza tatizo hili na pengine tuliondoshe kabisa.

Nikitoka katika kifungu hicho nije sasa katika mchango wangu kifungu chengine katika ukurasa wa 105, hapa panazungumziwa ufafanuzi. Nilikuwa nina baadhi ya maneno sikuyafahamu vizuri naomba Mhe. Waziri anisikilize vizuri halafu baadae kwenye majumuisho aweze kunisaidia. Na mawazo ninayotoa kama yatakuwa mazuri basi naomba yaingizwe katika mswada huu kwa lengo la kutengeneza ili mswada wetu uende vizuri.

Katika ufafanuzi huo ukurasa 106 neno linalosema ‘uchukuzi’ nitaomba nilisome lote halafu na mimi nitoe mchango wangu. ‘Uchukuzi’ hapa unasema “maana yake ni aina yoyote ya majumuisho yanayojumuisha aina yoyote ya ndege, gari, meli”. Hapa imekusudiwa kwamba uchukuzi pengine haya madawa ya kulevya inasababishwa au inajumuishwa na kuchukuliwa na vitu vitatu kama kwa ndege pengine kupitia *airport,* kwa gari barabarani na meli kupitia bandarini. Lakini mimi nadhani bado kama uchukuzi viko vitu bado vinachukua, si meli, ndege wala gari tu, lakini kuna vyombo vyengine kama vile vespa, pikipiki na vitu vyengine.

Mimi ningeomba hapa tungeongeza na vyombo vyengine vinavyohusika ikiwa vya moto au vya baridi, lakini naona sentensi hii haikukamilika. Nadhani tafsiri hapa bado ingeongeza maneno ikaweza kukaa sawa, la kama kisheria ndio inaandikwa hivi sina pingamizi, lakini bado vitu vinavyochukua madawa ya kulevya vingalipo. Sasa wataalamu watatafuta lugha itayofanana ya kukusanya vitu vyote ambavyo vinaweza kuchukua kutoka sehemu nyengine na kupeleka kwengine. Nadhani Mhe. Waziri kanifahamu na atakaa na wataalamu watalitizama, kama litakuwa na uzito basi watarekebisha na kuweka sawa, la njia ya kitaalamu ndio hivi imetosha sina tatizo.

Nikija kwenye ufafanuzi mwengine hapo hapo chini kuna neno ‘kulima’. Anasema kujumuisha kufukia mbegu, umwagaji wa mbegu, kuotesha, kulelea katika vitalu, halafu anasema utunzaji au uvunaji na pia unajumuisha

kutenganisha kasumba, majani na *kokeni*, mbangi na utomvu wake na mirungi kutoka katika mimea ambayo inapatikana. Mimi hapa tatizo langu ni hii ya mwanzo kwamba unajumuisha ufukiaji, nadhani kwa lugha zetu tunasema kupanda. Mtu yeyote ukimwambia unapanda anajua unapanda mbegu kama mpunga, kunde, mnazi, mchungwa na kadhalika, lakini ukisema kufukia ina maana unafukia shimo pengine limechimbwa la taka unalifukia.

Sasa nawaomba wataalamu wazidi kutizama lakini mimi kwa upande wangu naona tukitumia neno kupanda mbegu tutafahamu vizuri zaidi. Naomba wale wataalamu wa tafsiri wataangalia katika suala hilo ili tuweze kwenda vizuri.

Nikiendelea kwenye tafsiri nije ukurasa wa 108, hapa kuna tafsiri inayosema dawa za mkasumba wanaeleza maana. Pia nilitaka nitoe mawazo yangu kama kutakuwa kuna uwezekano litakaa sawa basi naomba Mhe. Waziri na wataalamu wake walifanyie kazi. Naomba ninukuu, "Dawa ya mkasumba dawa maana yake ni mkasumba ambao umepitia mchakato muhimu kwa ajili ya matumizi ya dawa". Mimi neno mchakato nimeona hapa halikuafiki, ningeomba niseme ifuatavyo kama itakuwa inaafiki basi Mhe. Waziri na wataalamu wake wanaweza wakaongeza. Neno 'mchakato' mimi naomba niliondoe niseme hivi, mkasumba maana yake ni mkasumba ambao unatengenezwa kwa ajili ya matumizi ya dawa, badili ya neno mchakato. Sasa naomba na hilo pia Mhe. Waziri na wataalamu tutizame lugha fasaha mchakato na kutengeneza. Hilo naomba pia kama halina madhara yoyote lingefanyiwa kazi kwa lengo la kuiboresha sheria yetu.

Pia nije kwenye ukurasa wa 110 kuna neno 'kuuza', naomba ninukuu na hapa pia niongeze ama nilitoe kabisa. Wanasema "Kuuza inajumuisha pendekezo la kuvutia, kutangaza au kuweka bayana kwa ajili ya kuuza". Sasa naona pendekezo la kuvutia kuna kitu kimekosekana. Kwa sababu kuuza ni kutangaza ikiwa kwa redio, gazeti ile inakuja kuuza, au kuweka bayana utapanga juu ya meza kama machungwa, tungule unauza, lakini ukisema pendekezo la kuvutia , nipite kusema suruali hii nzuri naona wataalamu na hapo waangalie pana kitu kimekosewa, ama mimi kwa mawazo yangu tungeanza tu, kuuza ni kutangaza na kuweka bayana kwa ajili ya kuuza. Naomba na hili wataalamu waliangalie kama kumekosewa kurekebishwe au wazo langu kama kuuza ndio hivi basi hili tungeliondoa tukaanza kutangaza au kuweka bayana kwa ajili ya kuuza.

Halafu mwisho katika tafsiri nahisi kuna neno tumelitumia lakini halikutafsiriwa na katika sheria limo. Naomba na hili kama itawezekana kutoa tafsiri yake si mbaya au kama imo ndani yake mimi sikuelewa pia sina tatizo. Lakini nilitaka nieleze tu kwamba ni kweli limesahauliwa basi lirekebishwe.

Mirungi imezungumzwa sehemu nyingi lakini mtu yeyote ukimwambia mirungi hasa wa Unguja atapata shida, lakini kwa Bara kwa kuwa wenzetu Wasomali wanatafuna sana kule hakuna tatizo. Sasa naomba na neno mirungi hili tungelifasiri kwenye ufafanuzi kwa kuwa huko ndani tumelitumia itakuwa hakuna baya kama itawezekana ili na mimi mtu wa Unguja nikiambiwa mirungi nijue kitu gani.

Nikitoka kwenye tafsiri nije sehemu ya pili ,Uanzishwaji wa Tume ya Mawaziri ya Kuratibu Udhibiti wa Madawa ya Kulevya. Mimi hapa nilikuwa nitoe mchango wangu katika huu uundaji wenyewe. Nimefanya hesabu hapa kifungu nambari nne hicho wametajwa wale mawaziri pamoja na maafisa ambao wamependekezwa kuunda tume hiyo. Nimehesabu mpaka mwisho ni watu 15 lakini hapo hapo kuna sekreterieti ya watu 11, sasa nikijumlisha napata watu 26. Kwa hivyo Mhe. Spika, nahisi ni mzigo mkubwa sana watu 26 kukaa kujadili kitu kimoja, kwanza mzigo wa gharama utakuwa mkubwa hawezi mtu kukaa bure itabidi lazima akikaa atafutiwe nauli kule aliko afike kwenye kikao, patahitajika chai pale wazee kulainisha koo, patatakiwa na cha mchana halafu mtu aondoke na bahasha mfukoni. Tunatengeneza lakini pia tutizame utengenezaji wetu, tuvunje pahala tunapoweza kujenga tusivunje eneo kubwa halafu tukajenga nusu.

Mimi wazo langu tume imekuwa kubwa sana ingekuwa angalau na watu 10 na hawa watendaji 5 ikawa 15 ingelikuwa inafaa. Kwa hivyo, kwa mawazo yangu mimi naona ikiwezekana kupunguzwa basi lingekuwa jambo la maana sana, lakini hivi ilivyo watu 15 halafu kuna kifungu hapa mbele tunaambiwa inawezekana kama kuna haja ya kuajiriwa maofisa kifungu cha 6 Mkurugenzi Mtendaji anapewa idhini na tume pia anaweza kuajiri maofisa kama anavyoona inafaa.

Sasa huko Mhe. Spika, wameshakuwa 26 halafu bado anaambiwa ikifaa aajiri na wengine, nadhani yote mawili hayo tuyatizame, kama ni kubwa sana basi tungefika kwenye 10 tume yenyewe na watano watendaji ili kuacha nafasi kama itakuwa kunatakiwa mtaalamu nje akaajiriwa ikawa wa 16 au 17. Mhe. Spika, naona mawazo yangu mimi nichangie hivyo, kwa sababu itasaidia sana katika kutekeleza haya mambo yetu ambayo yamekusudiwa.

Nikiingia mchango wangu wa pili ukurasa huo huo kazi za tume zimetajwa hapa nambari 7(1), mimi nitakuja kwenye kifungu cha (c). Hiki kinasema “Kuboresha na kuigiza sheria na kanuni za udhibiti madawa”. Mimi nadhani hapa pamerukwa kitu ama pamekosewa, nafikiri ingeliandikwa kuboresha na kusimamia sheria na kanuni za udhibiti madawa, neno hili kuingiza au kuigiza nadhani limeingia kwa makosa ama kama lipo nifahamishwe limekusudia maana gani? Lakini kila ninavyosoma mimi hainipi maana nzuri.

Sasa namuomba na hilo Mhe. Waziri alitizame, kama limerekebishwa kwenye karatasi ile sijaliona kwa sababu sikuwahi kuitizama kwa vile inalingana na huu mswada, karatasi ni nyingi sana kusoma miswada miwili utashindwa. Kwa hivyo, kama mengine yamerekebishwa humu tunaomba radhi sana tumeshindwa kuyapitia kwa sababu marekebisho ni makubwa mno.

Nikiendelea nije ukurasa wa 113 unaozungumzia vyanzo vya mapato ya tume. Hapa wenzangu wengi walizungumza juu ya suala hili lakini na mimi naona kwa vile nilijiandaa kulizungumza basi nilizungumze. Hapa panaseama hivi, (a) "Fedha zitazotengwa kwa tume na Baraza la Wawakilishi", nadhani hii ni kama bajeti itapita hapa. Lakini nyengine (b) inasema, "Rasilimali au vitu vya thamani vilivyofilisiwa…". Mimi nadhani na hili si baya lakini naona halina utaratibu mrefu.

Kwa sababu ninavyojua mali ya serikali gari iko katika wizara fulani au kitu kupigwa faini, kinatangazwa kuuzwa kikishauzwa kiende Hazina, kikifika huko kitiwe kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali halafu sisi tuombe kipite kwa Katibu Mkuu kiende kwa Waziri anayehusika na fedha kitoke kule kiende kwa Katibu Mkuu. Nadhnai kinachukua muda mrefu sana. Sasa hili moja katika kusaidia kazi hii kwa umuhimu tulionao mzunguko umekuwa mkubwa, nadhani zingetafutwa fedha maalum zikatiwa za kutosha kuendeshea mradi wetu, hii ingewekwa kama kitu ziada tu. Kwa sababu kazi zetu hizi ni ngumu na zinahitaji lazima patumiwe gharama kubwa iweze kutekelezeka sheria hii.

Pia kifungu nambari 3 kazi hiyo hiyo naomba ninukuu halafu nitoe mawazo yangu. Kinasema "Tume itasimamia makusanyo na matumizi ya fedha kwa ofisi, sekretarieti na itasimamia Mfuko wa taifa wa kupambana na madawa ya kulevya". Mimi hapa nadhani suala moja sikulipenda kimawazo yangu, tume ikusanye, isimamie matumizi, itakuwa mtu mwenyewe kwa mwenyewe inakuwa ngumu, lazima aweko na mtu mmoja tofauti.

Mimi nadhani kazi ya kukusanya tume tusiwape, wao watizame matumizi yanayotumika katika utendaji wa kazi na kuhoji kuwa je, zimetumika vipi na zimekwenda vipi, lakini tume huyo tumwambie kakusanye, tume wewe tumia, itakuwa tunawapa kazi nyingi sana bora tungewapa majukumu ya kutizamia sera yenyewe na kutizama hali inakwendaje katika utekelezaji wa shieria hii. Hilo wazo langu Mhe. Waziri kama litakuwa la maana sana na litasaidia sheria yetu basi naomba tuwapunguzie kazi Tume wabaki kwenye kuangalia matumizi lakini ukusanyaji tuuondoe.

Mhe. Spika, nije ukurasa wa 114 sehemu ya tatu unazungumzia mfuko vile vile. Lakini lengo langu huku chini namba 4 naomba ninukuu inasema

“Kutakuwa na ripoti ya matumzi ya tume itawasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi kwa taarifa.”

Lakini na huku nyuma kuna ripoti ya tume itawasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi, naona kuna ripoti mbili. Sasa naomba kama ni nia ya kuleta ripoti zote mbili basi zingechanganywa pahala pamoja, kwenye kifungu hiki cha 8 ingesema italetwa ripoti ya tume kwenye Baraza la Wawakilishi pamoja na matumizi yake, ili kuondosha kule kusema huku na kusema huku, inakuwa tuna jambo lile lile lakini tunaliandika mara mbili. Najua huku ni ripoti kubwa, lakini ripoti kubwa lazima ina matumizi kimahesabu ni vizuri unamaliza ripoti unaweka na matumizi yake.

Sasa naomba na hili wataalam kama litakuwa lina maana basi tungechanganya kwenye kifungu cha 8 tukaiondoa huku hii namba 4 tukaleta ripoti ya maelezo halafu na matumizi yake pale pale ndani ya ripoti ile. Nadhani itaondosha usumbufu ambao niliouhisi mimi unaweza ukatokezea.

Mhe. Spika, nikiendelea nije ukurasa wa 115 sehemu ya 4 “Marufuku kupatikanwa kwa madawa ya kulevya na kufanya biashara ya madawa ya kulevya pamoja na upandaji wa baadhi ya miti”.

Hapa nadhani kuna makosa na adhabu na imeelezwa hapa pengine anayelima bangi, mirungi kama atakuja kukamatwa basi atakuwa mkosa. Lakini mwenzangu mmoja jana hapa alisema kwamba nay eye alifanya wasi wasi kwamba serikali imeruhusiwa kulima baadhi ya vitu hivi kwa mahitaji maalum. Sasa mimi nimefanya wasi wasi kidogo, anaweza mtu akaambiwa akalime kwa nia hiyo iliyokusudiwa lakini huko huko porini akachukua nusu akenda kuuza. Pia na huyu akipatikana atakwenda kwenye adhabu hii.

Lakini pia nahisi kwamba katika adhabu huku mbele kuna adhabu ya mtu atakayekamatwa na unga kidogo na mtu atakayekamatwa na vidonge kidogo na hawa wanaolima utakuta adhabu zao zimepitana mno. Sasa sijui kwa nini wakati yote ni lengo moja kukataza madawa ya kulevya, lakini mmoja adhabu ndogo, mmoja adhabu kubwa. Mimi nadhani kwa kuwa tunataka hili jambo tuliondoshe kabisa tusibague adhabu. Kama kifungo cha maisha wote atakayekutwa na kete mbili, tatu maana ndio tunakomesha lisiwepo. Lakini tukisema atakayekuwa nacho kidogo tumpe adhabu ndogo, atakayekamatwa na begi zima apewe adhabu kubwa, itakuwa tunafanya mchezo haueleweki.

Kwa hivyo, nashauri mimi kwa mawazo yangu kama tumekusudia madawa kuyahamisha kabisa petu basi adhabu ziwe moja tu zote. Ukikutwa na kidonge, ikiwa umetumwa, ikiwa umekwenda kununua, ikiwa mwenye duka unauza adhabu iwe moja tu, kama miaka 40, kama milioni 40 ndio hiyo hiyo, ili

kuondosha kile kidogo na kikubwa. Wengi wataondoka kwenye kingi watakuja kwenye kidogo, kwa hiyo itakuwa kama tunahalalisha. Sasa Mhe. Spika, mimi kwa mawazo yangu suala hili adhabu iwe moja tu, ukikutwa na kidonge, ukikutwa na nyingi, nadhani hii itasaidia katika kuliondosha tatizo hili.

Mhe. Spika, kwa kuwa wenzangu mengi wameshayazungumza mimi nilikuwa nimebakiwa na hayo, naona nisichukue muda wako mwingi nitoe fursa kwa wenzangu. Kwa hivyo, namalizia kwa kusema mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu tunaunga mkono mswada huu.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi asubuhi hii ya leo kupata nafasi ya kuweza kutoa maoni yangu kuhusiana na mswada huu muhimu ambao uko mbele yetu. Mhe. Spika, mimi nataka nitofautiane na baadhi ya wenzangu wanaosema kwamba mswada huu umekuja kwa wakati muafaka. Tumechelewa sana, tumechelewa sana kwa sababu hali imekuwa ni mbaya mno huko nje na kumbe ni mbaya zaidi kuliko vile mimi nilivyokuwa nafikiria. Nimeogopa zaidi mchango wa Mhe. Hamza Hassan Juma jana alipoelezea hali yenyewe ilivyo.

Sasa kwa kweli masuala haya ya madawa ya kulevya ilikuwa kama hadithi ile ya nyoka huyooo anapita na apite, ilikuwa na apite kumbe sasa yumo ndani kajaa tele. Kwa hivyo, nasema huu mswada kwa kweli umechelewa sasa jukumu linaongezeka kwa wakubwa.

Mhe. Spika, wengi wamezungumza kwamba jukumu ni letu jumla jamala, nakubaliana nao nusu, lakini mimi nasema mzigo mkubwa zaidi uko kwa serikali na nitatoa sababu zangu.

Kabla sijaingia huko Mhe. Spika, napenda pia nichukue nafasi hii kumkumbuka sana na Mwenyezi Mungu amuwie radhi na amsamehe makosa yake mwenzetu Mhe. Amina Khamis Chifupa. Mwenyezi Mungu kamjaalia alikuwa na uhai mfupi sana, lakini alikuwa ngangari katika kuhakikisha anapigana sana na suala hili la madawa ya kulevya. Wakati wote yeye alikuwa hana nafasi, hana raha kwa kuona jinsi gani anaweza kuwatetea vijana wa taifa hili kuhusiana na janga hil la madawa ya kulevya.

Kwa hivyo, nimeona pia nay eye ana nafasi katika mswada huu ambao uko mbele yetu. Si kwa maana kwamba aingizwe ndani ya mswada lakini tumkumbuke kwamba nay eye alikuwa ni mpiganaji wa mstari wa mbele kutokana na adha hii tuliyonayo sasa hivi ya madawa ya kulevya. Mwenyezi Mungu amsamehe na sisi tulioko nyuma basi tuhakikishe kwamba tunalivalia njuga hili suala, ikiwezekana kuliondosha kabisa lakini kama haikuwezekana basi lipungue kwa asilimia kubwa.

Mhe. Spika, kwa sababu ya uzito wa mswada huu hata wale waliokuwa si wasemaji wamesema. Namshukuru sana mzee wangu Mhe. Burhan Saadat Haji nay eye alinyanyuka akatoa mchango wake kwa sababu ya uzito na adha ambayo inatukabili katika nchi yetu. Hii inaonesha umuhimu mkubwa uliokuwepo juu ya mswada huu.

Mhe. Spika, kama nilivyosema ni kwamba suala hili la madawa lina mizizi mirefu, kwa hiyo mimi katika mchango wangu zaidi nitachangia uhalisia wa hali halisi tuliyonayo na kidogo kidogo tu nitaingia kwenye huu mswada. Kwa sababu mambo mengi yameshazungumzwa lakini bado mengi yapo.

Mhe. Spika, Mhe. Aziza Nabahan Suleiman alizungumza sana jana hapa na kwa kweli yeye kama mzazi pamoja na sisi alikaribia kulia. Lakini nataka nimhakikishie kwamba hili suala si lake peke yake kadri ambavyo analiona. Kwa sababu ndio kama hiyo hadithi tunayoisema ya nyoka huyooo hujui saa ngapi ataingia mlangoni kwako, majumbani tunao watoto, tunao vijana, tunao ndugu zetu Mwenyezi Mungu awalinde na hawa ambao wameshapata matatizo Mwenyezi Mungu awahifadhi waweze kurudi.

Mhe. Spika, mimi ni miongoni mwa watu ambao nilichukua nafasi pia kumsaidia mwenzangu kwa nasaha mbali mbali kiasi ya uwezo wangu na si peke yangu tulikuwa wengi tu. Maana yake kama alivyozungumza mwenyewe amechukua jitihada ya kumpeleka kila pahala, sio tu humu ambamo kampeleka kama alivyosema Mombasa na kwengine, lakini na sisi wenziwe pia alituita jamani semeni na mwanangu, semeni na mtoto wenu na tulijitahidi. Kwa kweli mimi binafsi pia inaniuma nikisikia tayari amerudia tena, lakini ndio hali halisi ya hili suala.

Kama hatukukaa tukawa makini, napenda sana kutumia neno hili ambalo Mhe. Waziri Kiongozi nay eye analipenda sana. Tuwe makini katika kulishughulikia suala hili basi kwa kweli tutafika pahala nchi hii itakuwa hata viongozi wa kuiongoza hakuna kwa sababu baada yetu sisi ni hawa vijana wanaotufuata ambao sasa hivi wengi wao ndio hao wanaosinzia vichochoroni humu na wamepoteza dira, mwelekeo na sijui kama wao wenyewe wanayo hiyo tamaa, lakini wale wazee wanakuwa wana mwelekeo mdogo wa kuona hatima ya vijana wale. Kubwa tunakaa tunasikia wengine wanafariki kwa sababu ya kujidunga masindano haya, sijui kwa sababu yak u-expire wakati mwengine sumu yake inakuwa kali zaidi wanakufa haraka, labda wakemia wanaweza wakafahamu zaidi.

Mhe. Spika, nasema tuna jukumu kubwa na tuna kazi pevu kwa sababu sisi tunapokaa kupanga kwamba tutawakamata hawa walioko vichochoroni,

wenzetu wana kazi pevu kama wanapigana vita kuliko vile vita ambavyo viko Afghanistan au Baghdad.

Mhe. Spika, nitatoa mifano miwili mitatu. Katika wiki hii tuliyonayo siku mbili tatu za nyuma zilizopita kwa wale ambao wanaangalia vyombo vya habari tumeshuhudia kikioneshwa chombo kinaungua. Hadithi ya chombo kile au taarifa yake ni kwamba kilikuwa kimebeba madawa ya kulevya, baada ya kuona kuwa wameshaonekana na walikuwa na shehena, basi walichofanya waliitia moto na wenyewe wakajizamisha kuokoa maisha yao.

Mhe. Spika, si hilo tu, kuna *submarine* iliyokuwa na tani 10 za unga wa madawa hayo ya kulevya aina tofauti, ilionekana ikapigwa na Wamarekani. Sasa tuone ile juhudi ambayo serikali, ndio maana nasema pamoja na kwamba sote tunahusika lakini serikali ina jukumu kubwa. Serikali ya Marekani inatumia mapesa mengi mno, inatumia gharama kubwa sana katika kupigana na madawa haya. Kuna kundi moja wanafanya kama *SACCOS* hivi au ushirika wa watu wa unga, matajiri sana.

Katika hii kadhia ya juzi tu kuna madawa yaliyokamatwa katika tukio tu ni kilo 530, lakini hapo hapo zikakamatwa silaha za aina mbali mbali nzito 144. Isitoshe wana na magari ya kila aina, maana naeleza ule uwezo wa hawa watu wa madawa. Lakini jengine zaidi imekamatwa fedha taslim Mhe. Spika, dola za Kimarekani milioni 3.4, kwa kukisia unaweza ukasema bilioni 5 za Kitanzania.

Sasa hiyo ndio hali halisi ya hawa watu wenye biashara ya unga, inawezekana wanavuta lakini hawa magwiji, matajiri, billionaires pengine ni trillionaires. Hii ni sehemu moja tu inatajwa Mexico, hatujenda Bolivia, hatujenda Colombia huko ndio usiseme, shughuli iliyokuwepo Baghdad iko kule lakini katika hali ya kupiganiana madawa haya, ni vita kamili kwa maana ya vita sio hii kufukuzana vichochoroni tunayoizungumza.

Mhe. Spika, natoa hadithi hii ili tuone hili sakata linavyokwenda. Wengi wamezungumza kwamba chain inatoka mbali, ni hawa wenye hizi zana, ni hawa wenye haya mafedha na mambo kadhaa wa kadhaa ambayo watu wao wadogo wadogo ndio maana anaambiwa wewe ukenda ukirudi tu una chako milioni 50. Ile kuuchukua mzigo ukaufikisha, hujahangaika kuulima, sijui kuununua kwamba ule mzigo umefika pale unapotakiwa wala wewe si kazi yako nani atakuja kuuchukua, wewe umeshaambiwa ufikishe pahala fulani basi chako ni milioni 50 na kwenda mbele. Kwa hiyo, bado nasema kazi ni kubwa sana nah ii inaielemea serikali.

Wenzetu Wamarekani kundi lile la watu 30 sijui ndio ushirika wao ule wa watu wa madawa wamewekewa kikosi cha askari 50,000 wenye silaha nzito. Askari

50,000 wanapigana na watu 300 na hawawawezi. Kwa hiyo, tuone jinsi gani wale wala unga uwezo wao, masilaha yao, utajiri wao na zana zao.

Mhe. Spika, ndio maana pengine nchi kama China wao hawana mjadala ukikamatwa na kete yako moja tu ikipimwa ikitimia grams 25 sio kilo basi adhabu yako ni kifo, ikipungua tena una adhabu nyengine nzito, kali kali, zinaweza hizo hizo zikakumaliza ukafa vile vile.

Mhe. Spika, hii nataka niisemee kwamba kama nilivyozungumza wakati wa semina ile adhabu ya milioni 20, sisi milioni 20 tunaiona nyingi maana yake ndio kiinua mgongo cha wajumbe. Lakini ni kitu kidogo mno, Mhe. Andrew Chenge anaita vijisenti. Sasa bado hatujaweka adhabu ya watu hawa. Mimi sipendi sana adhabu ya kifo naona huu ni uwezo wa mtu mmoja tu, mtu akiamua kujiua mwenyewe hiari yake.

Lakini hebu jamani hawa wenye shughuli hizi afungwe maisha awe hatoki huko basi itakuwa watoto wetu watapona. Mimi sikubaliani na suala la kwamba vijana wanaovuta unga ndio wakamatwe kushtakiwa, nakubaliana wakamatwe tu lakini wapelekwe pahala. Imezungumzwa hapa wenzetu wana-rehabilitation centres wanaziita *REHAB* wawekwe.

Kweli ni gharama kama alivyoizungumza Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba mtu mmoja kwa mwezi dozi yake laki 4 kama sijasahau alivyosema jana hapa. Lakini nasema bado laki 4 kwa kuokoa nguvu kazi ya nchi hii, rasilimali, wanaita rasilimali watu siku hizi Kiswahili cha kisasa. Mhe. Spika, mimi nadhani bora tupoteze laki 4 lakini tuhakikishe tumewakusanya kwa maana ya kwamba wakae pahala watibiwe, wapate maadili mazuri, wafike pahala serikali iweze kuwatumia wale vijana kwa ajili ya kuendeleza maendeleo ya nchi hii kwa ajili ya maslahi yao binafsi, wazazi wao na jamii kwa jumla. Wakishawezekana wale wataweza kutuletea tija.

Mhe. Spika, mimi sikubaliani na utaratibu wa kwamba wanawekwa miezi 6 ikisha wanarudishwa makwao inakuwa ndio yale yale, unafuta ziro unaandika O umefanya nini, hujafanya kitu. Shughuli za kufanya zipo, kuna vikosi hivi mimi nasema hata havijatimia watu hawa hawa wanatosha, wakishakuwa wapo kwenye kambi yao hao hao watakuwa vikosi. Wao wao leo na kesho Mhe. Spika, hayawi hayawi huwa tunapozungumza tunatarajia kuna mafuta tutachimba, hawa hawa ndio watakaokuwa kwenye ajira hizo, sisi tunapiga kelele mpaka mambo yawe tu hapa na inshaallah yatakuwa.

Sasa hawa ndio watakaokuja kufanya kazi, patakapochimbwa mafuta kuna shughuli nyingi zinazotakiwa kufanywa. Pengine kutakuja na viwanda kutakuja na mambo chungu nzima, hawa hawa wengine akili zao nzuri wanasomesheka,

wanaweza kufahamu wakawa wataalam na viongozi wazuri tu. Iko mifano chungu nzima ya maprofesa ambao chanzo chao huko nyuma walikuwa watoto watukutu hawafai (*condemn*) lakini walionekana mmm tusiwaachie wakapotoka. Wakawekwa, wakasomeshwa, wakaweza, wakafanikiwa leo ni maprofesa.

Sasa mimi nasema bado tusione kwamba suala la watoto hawa vijana wetu wanaovuta madawa linaisha hivi hivi. Mhe. Spika, napenda sana kuchukua nafasi hii niiombe serikali iliyoko hapa ione jinsi gani watajipanga, jinsi gani watajipapatua, alimradi ala kulli hali viwepo vituo hivi. Mimi nasema si suala la kukaa mkaanza kupanga bajeti, kuna mambo yanafanywa kwa utaratibu wa kidharura, hili iwe ni kama maafa. Pakatafutwe wafadhili, pakafanywe mtakavyofanya vyovyote lakini vitu hivi viwepo, vijana wakamatwe kwa maana ya kuwekwa kambini kutibiwa kwa ajili ya kujiandaa sisi wenyewe kupata watu wa kuweza kuiendeleza hii nchi.

Sisi tunamalizika Mhe. Spika, miaka 40 huendi miaka 20 unakwenda 50, 60 safari. Miaka 60 kwenda mbele na hali hizi za maisha tulizonazo hatuna umri mrefu wa hivyo. Tuwachukue vijana hawa tuwafanyie vya kuwafanyia lakini tuhakikishe kwamba hawa vijana wanapona kwa maslahi ya nchi hii.

Mhe. Spika, dhamira ya serikali mimi nazungumza, sina hakika wala sitaki niwasemee kama ninavyosema ndivyo au sivyo lakini nachukua uzoefu, mimi naona hatujadhamiria. Hatujadhamiria kwa sababu nakumbuka kwenye miaka ya 96 mpaka 98 sina hakika mwaka upi, palikuwa na sakata na gazeti la Majira hapa, naam lilikuwa haliingii Zanzibar. Lilipigwa marufuku watu kumradhi Mhe. Spika na wajumbe wakisachiwa mpaka kwenye chupi, ndio na lilikuwa halipiti gazeti, anayelipata analisomea huko huko Tanganyika hapa hathubutu. Si bandarini, si uwanja wa ndege hupiti na gazeti la Majira na kama yako yaliyokuwa yakipita basi ndio yale aliyoyasema Mhe. Tafana jana, anapita na mzigo wake kwa sababu yeye mkubwa haulizwi, itakuwa walipitisha wao wakubwa, lakini kwa sisi wadogo huthubutu.

Mhe. Spika, kazi yah ii inawezekana iko katika namna hiyo na inatia mashaka kwamba iko hivyo. Kwa sababu miongoni mwa waliotajwa hapa mimi simjui hata mmoja. Lakini wapo watu wamesema kwamba kuna watu wanajulikana na wengine wamekwenda kujinasibu mbele ya kituo cha Polisi, sheha yupo, maafisa wapo, anasema muache huyu mimi ndio mwenye shughuli hii, kamtegemea nani huyu, anapo aliposhika hawezi kuwa na jeuri hiyo mtu. Sasa ikiwa hawa wanajulikana wametajwa na wawekezaji, wawekezaji humu ndani wanakuja vipi si tunawapokea, si kaja kutaka kuwekeza, kapitia wapi. Ana nini mpaka sisi iwe sheria zetu ziko chini mwekezaji yuko juu, mfanyabiashara sheria ziko chini yeye yuko juu, kuna nini hapa.

Sasa hapa Mhe. Spika, mimi ndio ninaposema hii tume yetu haifai kabisa. Kwa sababu ukiwa una mkubwa unamtegemea wakubwa wenyewe ndio hawa. Ukiitazama hii orodha Mhe. Spika, hii ni Baraza zima la Mapinduzi. Sasa wasi wasi wangu ni kwamba Baraza la Mapinduzi hili likija likishindwa kazi maana yake serikali yote haifai na nina wasi wasi huo kwamba ndivyo itakavyokuwa. Sasa ili isiwe hivyo kwa sababu itakuwa ni scandal ya dunia serikali imeshindwa kazi na mimi nadhani serikali kama hii yetu haifanani hasa kushindwa kazi Serikali ya Mapinduzi.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa na mapendekezo, mwenzangu aliyekaa kitako alisema kama tume ina watu wengi kahesabu yeye kaona 26, mimi namwambia pengine ni zaidi ya 26 kwa sababu hapa mwisho inasema na mtu mwengine yeyote ambaye Waziri Kiongozi ataona aingizwe. Kwa hiyo na mimi hapa jamaa yake ataona hata na huyu muingize, yapo maslahi kidogo. Anaweza asiingize mtu mmoja akaingiza watatu wanne kwa sababu tuko wengi sisi wapenzi wake eti.

Sasa mimi ushauri wangu kwanza tume iwe ndogo kadri itakavyowezekana na nina mapendekezo. Mhe. Spika, pendekezo langu hii tume tui-prun mpaka wabakie watu watano tu. Kwanza tutakuwa tumepunguza gharama ambazo ndio kilio kikubwa cha serikali yetu. Sio sisi tu, sasa hivi dunia nzima kila mtu analia ukata kwa hiyo hata hatutokuwa tumefanya la ajabu, tunajipunguzia gharama tufanye kazi yenye ufanisi. Kwa sababu kundi likiwa kubwa hili kila mtu Mhe. Spika, atamtegea mwenziwe. Utegezi inawezekana si wa makusudi kwamba mimi nategea lakini hawa mawaziri wana Rais wao yule wa Jamhuri kule akenda Marekani anawachukua. Sasa nyinyi mtakuwa mko kazini Mhe. Samia yuko Marekani na Rais Kikwete.

Wengine sasa hivi hawapo Waziri wa Elimu Mjumbe kwa mujibu wa mswada wetu huu yuko Ufaransa sijui. Sasa kweli hii kazi itawezekana watu wako Ufaransa, sijui wengine Marekani. Kwa maana hiyo, mawaziri majukumu yao ni mengi hatuwezi kuwazuia kwenda huko, tumeambiwa akenda huko akirudi misaada ipo, watakuja kutueleza siku moja misaada waliyoipata huko vizuri kwa sababu sasa hivi safari zimekuwa nyingi.

Sasa kwa sababu hiyo na hawa ni binadamu wanahitaji angalau wapate mwanya wa kupumzika na kuvuta pumzi basi hili jukumu tuwapunguzie, hii tume mawaziri wote watolewe na wabakie maafisa. Mhe. Waziri Kiongozi anajua wizara zake kwa mujibu wa serikali yake ilivyo na anawajua maafisa wake. Mimi najua kuna maafisa wenye uwezo mzuri tu wamesoma Alhamdulillah Mwenyezi Mungu awazidishie na ni watendaji wazuri, ni wafuatiliaji wazuri wanahitaji tu nyenzo.

Sasa Mhe. Spika, tume yetu hii iwe ni tume ya maafisa aweko afisa kutoka Mawasiliano, aweko afisa kutoka Wizara ya Afya, aweko afisa kutoka Wizara ya Utalii, kuwe na Mwanasheria na sio Mwanasheria Mkuu. Sisi hatuna njaa ya wanasheria tunao tele mpaka wengine wachanga hata hatujui tutawaweka wapi na wamesoma vizuri tu. Wengine nawaona hapa nikitazama kule. Aweko na afisa wa Polisi. Sasa hawa mabosi wao watasubiri ripoti. Ukiwachukua mabosi wote ukiwafanya wao ndio tume sisi wadogo tutasubiri shughuli iendelee ikifeli sijui itakuwaje. Sasa hawa maafisa ndio wawe tume wao watoe ripoti wakubwa wataipitia wataona wapi pana mapungufu, wapi paongezewe, wapi papunguziwe.

Lakini sitaki nikiondoshe kifungu cha mwisho cha Mhe. Waziri Kiongozi kwamba pindipo akiona kuna mtu anahitajika katika kazi hizi aweze kuingizwa baada ya wale watano lakini sio hili kundi zima ambalo itabidi wapewe basi wakenda kwenye shughuli zao waingie.

Mhe. Spika, nimesikitika jana katika wachangiaji hapa walipozungumza suala la wale mbwa kwamba kumbe wameshakufa wote. Mimi wala sikufikiria kama wamekuja wanaumwa hawa, nimerudi kule kule kwenye ufisadi kwamba inawezekana hawa mbwa wataleta nuksi. Maana yake binadamu anaweza akasikia harufu akajifanya pua zake hazishiki lakini mbwa hana habari hiyo, akinusa maana yake anakung'ang'ania hapo hapo. Jamani mbona haondoki huyu kwenye koti la mheshimiwa kumbe vipo vitu.

Lakini kama mimi nikitumwa tena sahibu yangu namuonea haya, namuonea tabu nitajibaraguza maneno ya Kiswahili niseme nimekwenda lakini sijaona kitu. Pengine ili nihakikishe kama sijaona kitu namtumia message maana yake nikipiga simu nitaonekana eti, nitamtumia message nimwambie bwana wewe tunakuja huko time fulani siku fulani kaa vizuri. Kishafahamu maneno ya kijitu kizima hayo, atapeleka kwa jirani yake, kwa bibi yake ambako hakuna mtu yeyote atakayefikiria kwa bibi yule san asana ukenda kusachi utakuta ugoro kumbe kishakwenda kuwekewa vitu pale akiba watu wamemaliza shughuli zao upelelezi ukisha shughuli inaendelea.

Sasa Mhe. Spika, mimi nasema nimesikia hapa kama majibwa hawa wana gharama kubwa sana na kweli mtaka uzuri lazima udhurike, huwezi tu wewe unataka kufanya jambo lako kubwa halafu uambiwe utoe pesa mbili au pesa nane, wengine pengine hawajui pesa nane nini lakini habari ndio hiyo zilikuwepo hizi pesa.

Kwa hiyo, itabidi tutumie, itabidi tugharamike ili tufanikiwe. Kwa hiyo, hawa majibwa nao ni muhimu kwa nao. Katika kuwa nao tumeambiwa kumbe mpaka

watu ambao wanaweza kuwashughulikia vizuri chakula chao na kila kitu itabidi na wao pia wawe wanawashughulikia vyenginevyo waje watupe maelezo tufahamu vizuri kwa nini alikufa? Kwa sababu hii kunusa ni tabia yao wala mimi siamini kwamba katika kipindi hicho kifupi ile kunusa ndio imewapelekea kufa, kwa sababu naijua *physiology* ya mbwa.

Mhe. Spika, *physiology* ya mbwa Mwenyezi Mungu kamuumba yeye kusikia harufu ni kazi yake kuliko kiumbe chengine chochote Mhe. Spika, wala hahitaji kupeleka pua yake pale kwenye mzigo. Mhe. Spika, hapa ukumbini tulipo kama kutakuwa na kipembe kimefichwa kishuwea kiduchu, wenyewe wanaita pipi basi yule mbwa akiingia tu hapa basi moja kwa moja atakwenda kuonesha kwamba ni hapa, kwa sababu keshahisi kwamba eneo hili kuna nini?

Kwa hivyo, sio kweli kama mbwa huyo ndio kanusa ikampelekea yeye kufa kwa kipindi hicho kifupi. Mimi *scientifically* kitu hicho sikubali, lazima kuna kitu chengine cha ziada. Aidha alinusisha nyingi kwa makusudi ikawa ni *overdose*. *Overdose* Mhe. Spika, hata mimi nikija nikipigwa *overdose* ya dawa sibakii eti, itakujakuwa mbwa, mbwa na yeye anaroho vile vile.

Kwa hivyo, kuwe na wale watunzaji mbwa dhamana, anapokufa mbwa atupe maelezo, kwa nini mbwa kafa na maelezo yake yafanane na maelezo ya daktari atakayemfanyia *postmortem*. Mhe. Waziri utakapokuja hapa napenda sana na ikiwa hujaitafuta basi uitafute taarifa je, majibwa hawa walipokufa walikwenda kufanyiwa *postmortem* na maelezo yalikuwa ni ya kitu gani? Ni lazima wafanyiwe Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi nimefanya kazi *vetnary* watu walikuwa wakiwaleta mbwa. Kulikuwa na mbwa akiitwa Cpl. John aliletwa na wakati mwengine wanakufa kizembe zembe tu majibwa hawa, pengine hashibi, kilo tano yake ya nyama inayopelekwa watu na wao wanachukua kitoweo humo humo, ndio! Sasa utamuacha mtu na njaa si mwisho anakufa na mbwa ni hivyo hivyo. Kwa hivyo, ikiwa *ration* yake ni kilo zake tano basi apewe, usimuuwe kwa njaa ukatuambia kafa kwa sababu kanusa madawa, hawezi kuvuta *dose* hiyo ya kumuua, vyenginevyo iwe kadungwa au kanukishwa kwa makusudi au vipi? Kwa hivyo, tuje tuelezwe kwamba hao mbwa walipokufa walifanyiwa *postmortem* na je majibu yao yalikuwa ni nini? Itakuwa ni ngumu sana, lakini hata mimi ningeletewa nikaisoma basi ningeona vizuri zaidi, maana yake nafahamu.

Kwa hivyo, haya yote Mhe. Spika, nilikuwa nazungumza kwamba tuone jinsi gani tatizo hili ukubwa wake, mazingira yake na kazi ngumu ambayo sisi imetuelekea. Lakini itakuwa ni nyepesi kwa kuwa na dhamira ya kweli,

itakuwa nyepesi kwa kutokwepa gharama, itakuwa nyepesi kwa kujaribu kudogosha mambo ambayo ukubwa wake hayana faida.

Mhe. Spika, mfano mzuri ni hii tume iliyoundwa hapa kama mkutano wa hadhara, basi iwe ndogo kadiri itakavyowezekana, kwa maana ile ile ya kwamba tunahitaji kuwa na ufanisi na pia tunahitaji kupunguza gharama ambazo si za lazima. Kikao cha watu wote hawa kitaambiwa kwa siku pengine kimechukua shilingi milioni 2 na wakipungua tutaambiwa shilingi 300,000/=.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa na mimi nafasi ya kuzungumza machache kuhusiana na mswada huu. Haya ni maoni yangu kwa maana ya kujenga. Sikwenda moja kwa moja kwenye mswada, lakini nilitaka kuelezea hali halisi ambayo tunayo. Naiomba sana Serikali iwe *very serious* katika suala hili na wala isiwe kwamba tukimaliza hapa sheria ya wanaounga mkono wamenyanyua mikono, kisha wengine wameacha mikono kisha tukafunga vitabu hivi ikawa watoto wetu wanaendelea kusinzia huko barabarani. Tunataka kuona sheria inafanya kazi na kwa sababu imetajwa kwamba wapo wanaojulikana na wapo waliokwenda kujinasibu kwenye vituo, basi tunataka tuone kuwa sheria imechukua mkondo wake. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ashura Abeid Faraji: Mhe. Spika, kwanza kabisa natoa shukurani zangu za dhati na mimi kunipa fursa hii nikatoa nasaha zangu za kijitu kizima. Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba leo tunafika hapa sote hatujambo, japo wengine tunavihoma haviondoki ni vya daima lakini tunashukuru.

Mhe. Spika, wenzangu wameyasema mengi sana kuhusu mambo ya madawa ya kulevya. Lakini na mimi nitowe nasaha zangu kidogo kwamba ‘uchungu wa mwana aujuae mzazi’. Mhe. Spika, vijana wetu wengi wanapotea na wanapoteza roho zao kwa madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, kilichobakia ni Serikali. Uwezo wanao, nguvu wanazo na nia wanazo wafanye kadiri ya uwezo wao ili yaweze kuzuiwa haya madawa ya kulevya. Mhe. Spika, nasema hivyo, kwa sababu waliambiwa watu hapa, na zikatoka nasaha na amri kwamba hawa wanaoendesha vespa wote wawe wanavaa makofia, kwa hivyo wote sasa wanavaa makofia, hawaendi vichwa wazi. Kwa nini Serikali isijitahidi karidi ya uwezo wake ikayazuia haya madawa ya kulevya?

Mhe. Spika, hapana anayehukumiwa zikikamatwa dawa hizo, hakuna anayefungwa zikikamatwa dawa hizo. Mhe. Spika, naomba watoto wetu wengi watakaokuwa viongozi wazuri watakaokuja mwaka wa mwakani, tufanye jitihada ili tuwaokowe watoto wetu na wawe watoto wazuri. Mimi naomba

kifunguliwe chuo cha Quraan cha wale watoto wanaokula madawa ya kulevya wote waende wakafungiwe mula na wasomeshwe Quraan na kusomeshwe elimu ya maana ya madawa ya kulevya. Labda Mwenyezi Mungu anaweza kuwajaalia watoto wale wakawa haijambo kidogo, kwa sababu watoto wengine wameshaanza kwenda.

Mhe. Spika, mimi nina mtoto wa mjukuu wa kaka yangu alikuwa akila madawa ya kulevya mpaka akawa anagaragara, mpaka herini za mkewe alikuwa akiziiba na kuziuza. Sasa akampata mweziwe mmoja akamwambia twenzetu Morogoro ukatembee. Alipofika kule akamtia kwenye chuo cha Quraan, sasa kawa Ustadhi wa ajabu! Hata apate ile tende ya kuwa yeye kapewa msaada basi na mimi ananiletea. Namshukuru Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, na sisi tusikae tu kama ndio wazazi, uchungu wa mwana aujuae mzazi, watoto wetu wanapotea vibaya.

Mhe. Spika, nchi yoyote ni lazima iwe na wazee pamoja na vijana. Ingawa wao watoto wetu wanatuambia dingi hilo limepitwa na wakati, lakini si tupo tunawasaidia! Kwa hivyo, naomba Serikali uwezo wanao, lakini kesi hizi zikifika kule ndio basi, halafu haya madawa yote yanayokamatwa yanakwenda wapi, yanachimbiwa shimo gani na yanachomwa moto sehemu gani? Ili sisi tuoneshwe kwenye TV. Lakini pengine yatachomwa majani ya mgomba halafu madawa yawepo vile vile. *(Vicheko)*.

Mhe. Spika, mimi naona huruma sana nikipita njiani nawaona wale wajukuu zangu wamekaa wameregea mwili mzima, maskini Mwenyezi Mungu atawavua katika balaa hilo awaweke kwenye kheri *Inshaallah*.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nilikuwa natoa nasaha zangu za kijitu kizima, tujitahidi wazee na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar uwezo mkubwa ulionao. Kwa sababu yaliyopita duniani si hayo tu ni mengi na mengineyo na wanayazuia hayaji tena. Serikali ya Zanzibar ilikuwa Serikali ya ukoloni lazima tupite huko kidogo. Serikali ya Ukoloni ilikuwa haina vyuo, wazee wetu wakifa tu hivi hivi hawajasalipo. Lakini baada ya kupata Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuna vyuo, kuna Misikiti na kuna kila kitu. Siku hizi kuna wanawake wa aina tatu sasa.

Mhe. Spika, utamuona mwanamke na mtandio wake mpaka chini kama nilivyojitanda mimi, kuna wengine wenyewe wanaipenda dunia wako huru vile vile na kuna wengine wanavaa kama desturi zao za zamani. Kwa hivyo, Serikali inao uwezo mkubwa, tunaomba. Nasema tena kwa mara ya tatu. Mhe. Waziri Kiongozi upo wee mwanangu tuokowe, waokowe vijana hawa.

Mhe. Spika, unajua vijana wengi wanaondoka ndani ya dunia na hizo kura tutazipata wapi? Wanakura za kutosha. Ikiwa ni za kuiba, ikiwa ni za kuchomoa na ikiwa ni za halali, lakini wanazo. Kwa hivyo, tunaomba Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar iwaokowe watoto wetu.

Mhe. Spika, sina mengi isipokuwa na mimi nilikuwa natoa nasaha zangu za kijitu kizima. Mwenyezi Mungu atupe kila lenye kheri, watoto wetu Mwenyezi Mungu awape moyo na sio watoto tu hata watu wazima wanakula haya lakini wanajificha ficha na wao pia Mwenyezi Mungu awaelekeze kuzuri. Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Hija Hassan Hija: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kutoa mawazo yangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani, nitakuwa na mchango ambao sio mkubwa sana.

Mhe. Spika, nikianza mchango wangu nianze kwenye tume ya mawaziri, moja kwa moja nimuunge mkono Mhe. Zakiya Omar. Kwa kweli mimi binafsi sioni sababu ya kuwa na tume kiasi kile, hasa kwa vile wajumbe wa tume ile ndio Serikali. Kwa mtazamo wangu nadhani kwamba Serikali hapa inakusudia kufanya mchezo. Huwezi kuweka Serikali kuwa ndio watu wa tume baadae wakifanya kosa maana yake nani sasa awafuatilie. Unasema kwamba Waziri Kiongozi ndio awe Mwenyekiti, na yeye ni mwanadamu je, akifanya kosa ni nani amfuatilie?

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mtazamo wangu ni kwamba tuwaamini watendaji wetu, tuwaamini maafisa wetu na tuwaamini wasomi wetu kwamba ikiwa kuna uadilifu basi hawa maafisa wetu wanaweza kufanyakazi. Nadhani Serikali hapa ione busara kwamba watendaji maafisa wa Serikali wenye sifa ya elimu na uaminifu basi tuwape jukumu na Serikali iangalie, ili wakifanya kosa basi na Serikali iweze kuwawajibisha. Lakini kumweka Mhe. Waziri Kiongozi na mawaziri na wao ni wanadamu na watu wenye madawa ya kulevya ndio hasa wanawataka wale Masheikh na viongozi ili wawashawishi, hawa viongozi watashawishiwa na mchezo utaendelea maisha wala hatufanikiwi.

Kwa hivyo, mimi nasema kwamba ni lazima maafisa wa Serikali wapewe jukumu na Serikali ikae pembeni ili iangalie hili jukumu kwa kufuatilia.

Mhe. Spika, jengine kwenye udhaifu wa tume ya mawaziri ninaouona ni masuala ya kikao. Mswada unasema kwamba watafanya vikao kila baada ya miezi minne. Nina wasi wasi kwa suala la kifedha, hata kama utawaweka watu wazuri kiasi gani ikiwa Serikali haikuiwezesha kifedha maana yake vikao havitafanyika. Nasema hivi kwa sababu nina mfano mzuri katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, mwaka jana tumepitisha mswada hapa . Mswada wa

sheria na tukaidhinisha kwamba iundwe bodi ya dawa asilia. Mhe. Spika, taarifa ambayo ninayo ni kwamba bodi ile imeteuliwa mwaka jana mwezi wa 5 na mswada unasema wafanye vikao kila baada ya miezi 3 hadi leo hawajafanya kikao hata kimoja.

Mhe.Spika, kwa msimamo huu na kwa mtindo huu na hii tume ya mawaziri basi vikao havitafanywa kwa sababu fedha hazitapatikana. Mfano huu wa bodi ya madawa asilia hadi leo hakuna kikao licha ya kwamba bajeti imepitishwa na wamekaa wanasubiri hadithi tu. Kwa hivyo, na hii tume ya mawaziri itapitishwa lakini hakuna kikao ambacho kitafanywa na halafu na maelezo ya mawaziri kuja Barazani yatakuwa ni maelezo ya kuchekesha tu. Kwa sababu madamu hawana fedha hawatomudu kufanya vikao. Kwa hivyo, mimi nasaha zangu ni kwamba Serikali kama kweli imedhamiria kulifanya hili suala basi fedha zipatikane kwa mujibu wa taratibu zilivyopangwa.

Mhe. Spika, jengine kwenye tume hii ya mawaziri ni vyanzo vya mapato. Mhe. Spika, mimi nimeshangazwa kwamba Serikali wanakataa madawa ya kulevya, lakini wanataka mwenye madawa ya kulevya akikamatwa waweze kumfilisi. Huo ni ushawishi. Unapomwambia mtu ukikamatwa na madawa ya kulevya basi nyumba yako moja itauzwa, nadhani Serikali inafanya mchezo. Nadhani inalenga kupata mapato sio kukemea makosa.

Mhe. Spika, nasema kwamba chanzo hiki cha kupata ruzuku kwa wafadhili na wahisani ni dalili na ni chanzo cha rushwa, na ndio lengo la Serikali kwamba wanakusudia matajiri wenye kuleta madawa wawape mwanya wa kutoa rushwa. Hivi tajiri gani mwenye madawa ya kulevya ukimwambia alete shilingi milioni 20 ruzuku asilete, wakati anajua mfuko mmoja wa madawa ya kulevya ni shilingi milioni 300. kwa hivyo, mimi nasema chanzo hiki ni kibaya hakifai na itakuwa watu wanakataa nyama ya nguruwe lakini mchuzi wanakunywa, ni kichekesho Mhe. Spika.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kama kweli tuko *serious*, serikali haiwezi kuchukua chanzo hiki cha ruzuku na michango mbali mbali ya mauzo ya wale wenye madawa ya kulevya ni chanzo cha rushwa na kwa kweli tutakuwa hatufanikiwi. Ushauri wangu ni kwamba jambo hili Serikali walipigie kifua wenyewe, mfuko wa Serikali ugharamikie moja kwa moja kwenye suala hili la tume ya mawaziri, na tuache kupokea michango,rushwa na mambo mengine. Hii michango na mambo mengine tusubiri kwenye masuala ya kisiasa tuchangiwe huko. Watu watugawie kofia, fulana na viatu. Lakini masuala ya madawa ya kulevya tukatae moja kwa moja michango na ruzuku za watu binafsi.

Mhe. Spika, nasema hivi kwa sababu juzi mwanasheria alipokuwa akitusomesha kwenye semina, alisema sheria yetu ya sasa haina meno, lakini

alisahau kutuambia kwamba sheria ya sasa imetawaliwa na rushwa na mambo mengine, hii ndio mianya ya rushwa iliomo ndani ya sheria hizi. Mimi nasema ikiwa tumekusudia kupambana na suala hili, basi tupige vita kwa nguvu zote masuala ya rushwa na vishawishi vyengine vitakavyowafanya wananchi washawishike.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningechangia ni suala zima la mkemia mkuu wa Serikali. Mhe. Spika, sisi kama ni wawakilishi wa wananchi tumekuwa tukilalamika kwamba mkemia mkuu wa Serikali hafanyi kazi ipasavyo. Lakini tumekuwa tukilalamika suala hili bila ya kufanya utafiti, inawezekana kuna udhaifu unaomfanya asifanye kazi zake vizuri.

Mhe. Spika, taarifa ambazo ninazo hadi leo mkemia mkuu hapa Zanzibar hayupo na aliyepo anakaimu kwa muda wa miaka 2. Sasa mtu unamfanya akaimu kazi hii kwa muda wa miaka 2 maana yake unamfanya asiwe na maamuzi. Kwa hivyo, ushauri wangu ni kwamba kama kweli Serikali iko makini, basi huyu aliyekaimu kwa muda wa miaka 2 kuanzia leo au kesho basi aidhinishwe kuwa mkemia mkuu wa Serikali, vyenginevyo unamfanya asiwe na meno, hili jukumu sio lake.

Mhe. Spika, kumfanya mtu akaimu kwa muda wa miaka 2 ni udhaifu wa utendaji. Mhe. Spika, naiomba Serikali kabisa huyu mtu wamuidhinishe awe mkemia mkuu wa Serikali kuanzia leo tena sio zaidi ya kesho, kama kweli lengo ni kupambana na madawa ya kulevya. Ukimwambia mtu akaimu maana yake na bahati mbaya huyu mtu anayekaimu pengine hapewi posho wala stahiki zake, yeye yupo tu jina la kaimu mkemia mkuu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, huu ni udhaifu na udhaifu huu kwa kweli Serikali isipouangalia maana yake wanatuonesha dhahiri kwamba huu mswada ni mchezo wa kuigiza na hauna mafanikio yoyote. Ikiwa mkemia mkuu hajaidhinishwa wala hapewi posho zake zinazostahiki, sijui utamuambiaje achunguze madawa ya kulevya? Hata ningekuwa ni mimi ningekuambia ni unga wa muhogo! Kwa sababu ni lazima nipate stahiki zangu ndio nilinde haki ya watu. Huwezi haki yako kuipoteza halafu nikalinde haki ya mtu mwengine.

Mhe. Spika, naomba sana mkemia mkuu aidhinishwe na apewe stahiki zake ili aweze kupambana na suala zima la madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningechangia masuala ya adhabu na makosa mbali mbali. Juzi mwanasheria alitufahamisha kwamba mswada huu unahimiza kwamba sasa hivi kosa likipatikana, basi uchunguzi ufanywe haraka. Mhe. Spika, nadhani kwa mtazamo wangu na hiyo haraka bado ina kificho sana, haraka hii itakuwa ni kwa yule mnyonge. Lakini haraka kwa maana ya tafsiri

ya kimahakama inawezekana ni miezi mitatu, minne au mitano. Sasa mfanyabiashara mwenye mali unamweka na madawa ya kulevya miezi mitano au sita ndio haraka yake hiyo, ni dhahiri kosa halipatikani.

Mhe. Spika, ushauri wangu ni kwamba huu mswada utuambie je, ni masaa mangapi uchunguzi ufanywe na ukweli upatikane? Wasi wasi wangu ni kwamba mtu mnyonge haraka yake itakuwa nusu saa lakini tajiri haraka yake itakuwa ni miezi sita!

Mhe. Spika, kwa hapa nataka mswada useme ni masaa mangapi uchunguzi ufanywe, nchi hii ni ndogo na ni ya watu kidogo sana, kwa hivyo tupate masaa mangapi ili uchunguzi ufanywe na ukweli upatikane? Lakini haraka tu nadhani sio neno zuri la kutumia kwenye sheria. Wafanyabiashara ni wajanja kwa hivyo na hiyo haraka ni vigumu sana kulitafsiri. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba tuambiwe ni masaa mangapi uchunguzi utafanywa na kosa libainike kama ni kosa au sio kosa?

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka nichangie kwa ufupi sana ni suala zima la adhabu. Mswada huu umependekeza adhabu nyingi sana ikiwa ni pamoja faini na kifungo cha maisha. Mhe. Spika, nadhani tusizunguke sana, sheria hutungwa na wanadamu na kutumiwa na wanadamu. Juzi nimeona kwenye televisheni kwamba wale waliotuhumiwa na kupatikana kosa la mauaji ya albino wamehukumiwa kitanzi hadi kufa. Sasa mimi nalinganisha na ukubwa wa lile tatizo na madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, mimi nasema kwamba ikiwa kweli tumekusudia kupambana. Mfanyabiashara ukimwambia alipe shilingi milioni 20 au vyenginevyo, nina hakika ni masihara. Tuamuwe kabisa mwenye kuleta madawa ya kulevya na mwenye kiwanda basi tuwanyonge, kwa sababu hata Quraan imesema kwamba ulevi ni mama wa maasi, mtu akilewa maana yake atazini, ataiba na atafanya kila kitu. Sasa tukimwambia wewe lete ulevi halafu utupige shilingi milioni 20, basi wataleta hapa kila siku na watu pesa wanazo. Kwa hivyo, tungeamua kabisa kwamba mwenye kuleta madawa ya kulevya na mwenye kiwanda basi tuwanyonge. Mwenye kulewa ndio tumpeleke mahakamani tumfunge miaka 20 au 30.

Lakini Mhe. Spika, ukisema kwamba basi tuwapige faini, maana yake ni faini au kifungo. Mhe. Spika, hawa watu pesa wanazo watatoa tu kila siku na wala hatofungwa mtu katika nchi hii. Mhe. Spika, mimi naomba mswada huu usiwaogope Wazanzibari, tuwanyonge watu wenyekuleta madawa ya kulevya na tuwafanyie wazi wazi. Kwa sababu tukimpata mmoja basi na wengine hawataleta tena madawa ya kulevya. Tukisema kwamba tuwapeleke gerezani.

Mhe. Spika, tumeona hapa mabenki yanaibiwa na watu wanatiwa jela siku moja na siku ya pili wanatembea na ma-Prado.

Mhe. Spika, huu ni ukweli kwamba watu hawatofungwa na dhahiri watu wataendelea kusinzia na kutumwangia maradhi huko mitaani. Mtu huyu mwenye madawa ya kulevya anadiriki kuwapiga sindano watoto wadogo, masindano yale pengine yana Ukimwi. Sasa unamfanya mtu asababishe madhara kwa watu wengine kwa nini yeye asiuliwe. Mhe. Spika, nadhani mswada usiogope na utekeleze tume hiyo.

Mhe. Spika, baada ya hayo nitowe masikitiko yangu kwamba jana kuna mwananchi wangu mmoja wa Jimbo langu la Kiwani ambaye yuko hapa Unguja, alipigwa kisu cha kwenye moyo kwa sababu ya ulevi. Walikwenda kulewa pahala panajulikana, lakini bahati mbaya hadi leo mpigaji bado hajakamatwa na alipigwa kisu hadharani. Ni udhaifu wa watendaji, mtu kampiga kisu mwenziwe hadharani tena kilabuni na watu wapo, lakini hakuna mtu aliyekamatwa mpaka leo. Kwa hivyo, wasi wasi huu wa kuwa mtu anauwa hakamatwi je mwenye mafedha ambaye analeta madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, maeneo ambayo madawa ya kulevya nina hakika watu wanayajua, kuanzia Pemba na Unguja hii watu wanayajua. Kwa hivyo, mimi ningeridhika na ningeunga mkono mswada huu kama sheria ingesema moja kwa moja tuwauwe. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukuwe nafasi hii kumshukuru Allah Subhanahu Wataala, kwa kunipa uzima na kuweza kusimama katika kiriri cha Baraza lako ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye mswada huu ambao uko mbele yetu.

Mhe. Spika, dunia yetu sasa hivi imepata mitihani mitano mikubwa. Moja ni mtikisiko wa uchumi duniani na hii imewakumba wakubwa na wadogo, hata sisi huku tunaoambiwa nchi za dunia ya tatu pia imetukumba.

Mhe. Spika, changamoto ya pili ni kuzidi kwa joto duniani. Asubuhi Mhe. Waziri katuambia kuna nchi ambazo zimeganda mabarafu kwa miaka chungu nzima, mabarafu yanayayuka yanaingia baharini, kuna baadhi ya visiwa tayari vimeshaanza kuonesha adhari ya kutoweka, lakini na kwetu huko kuna mafungu ambayo wavuvi walikuwa wakiyatumia wanasema sasa yameshafunikwa na maji.

Mhe. Spika, changamoto la tatu ni upungufu wa chakula duniani. Nilikuwa nikisikiliza taarifa ya *FAO*, wanasema karibu watu milioni 12 watakufa njaa

kama kilimo hakikupewa kipaumbele. Pamoja na kilimo kupewa kipaumbele suala la ukame pamoja na mafuriko nalo limeleta machafuko makubwa.

Changamoto la nne ambayo imekumba dunia Mhe. Spika, ni tatizo la madawa ya kulevya. Hili tatizo hatuna sisi tu hapa, ni tatizo la dunia nzima. Kuna nchi imetunga sheria kali kali.

Kwa mfano Saudi Arabia ukikamatwa na kilogram moja tu ya madawa ya kulevya basi kichwa chako ndio halali yao.

Mhe. Spika, changamoto la tano, ni suala la Ukimwi. Sasa hizi ndio *challenge* tano ambazo zimeikumba dunia. Ili kukabiliana nazo panahitajika ushirikiano wa kimataifa na wa kitaifa.

Mhe. Spika, katika *challenge* hizi nafikiri mbili tunaziweza. Zanzibar bila ya madawa ya kulevya inawezekana na Zanzibar bila Ukimwi inawezekana. Lakini itawezekana tu pale ambapo tutaungana katika suala zima la kusimamia. Zaidi mswada uliokuwepo mbele yetu kuweza kuusimamia vizuri ili ukaweza kufanya kazi.

Mhe. Spika, mimi nataka niungane na wale ambao wamesema kwamba mswada huu umechelewa sana kuja. Kama tulihisi mswada ule wa mwaka 2003 ulikuwa haufanyi kazi, basi ilikuwa haraka haraka tulete mswada huu.

Mhe. Spika, nasema umechelewa kwa sababu nitaelezea matatizo ambayo jamii inaikumba kutokana na madawa ya kulevya. Mhe. Spika, mtaani kwangu Miembeni kumesemwa sana hapa, jana nilihesabu imesemwa kama mara saba. Lakini tatizo la madawa haya ya kulevya haliko Miembeni tu, sasa hivi limejaa shehia zote, hata mashamba tayari hili tatizo limeshaanza kufika.

Mhe. Spika, nasema mswaada huu umechelewa, kwa sababu nitatoa mambo sita ambayo nimeyashuhudia mimi mwenyewe. Moja Mhe. Spika, kuna familia moja ya watu watano ilikuwa Miembeni, familia hii ilikuwa ina watoto wanne wanaume, mmoja mwanamke na mama yao. Bahati mbaya mtoto wa kwanza alipata ajali ya gari akafa, lakini haikutimia hata mwaka mtoto wa pili nae akafa kwa kuzidiwa na madawa ya kulevya, kapiga madawa kalala, kaamka asubuhi maiti.

Haikutimia hata miezi mitatu mtoto wa tatu kaokotwa uchochoroni, sindano moja imemganda mkononi na mbili anazo mfukoni. Dada mtu ndugu yao mwanamke peke yake kusikia ndugu yake kaokotwa uchochoroni kapata *pressure* kapelekwa hospitali baada ya wiki mbili kafa. Mama mtu nae kapanda *pressure* kupelekwa hospitali haikuchukua wiki kafa. Utakuta familia hii yote

imesambaratika kabakia kijana mmoja nae akaona na mimi nisije kufa akakimbia akenda zake majuu huko kutafuta maisha. Hii ni athari iliyoikumba familia hii kutokana na madawa ya kulevya.

La pili Mhe. Spika, nilishuhudia kuna mama mmoja amezaa mtoto mmoja tu na bahati mbaya mtoto huyu amejitia kwenye madawa ya kulevya. Alikamatwa akawa yuko Kiinua miguu. Mama mtu asubuhi kachukua chai anampelekea mwanawe ilikuwa kawaida yake asubuhi na mchana anampelekea chai na chakula, maana mwanawe ndio huyo huyo kama pua, mmoja tu.

Bahati mbaya akajikata bati kwenye mguu wakati anakwenda kupeleka chai, donda lile limekua kumbe alikuwa na ugonjwa wa sukari, hatimaye mama huyu ikabidi akatwe mguu. Siku ya kukatwa mguu tukafanya maarifa kwenda kumuomba huyu kijana akamshuhudie mama yake anakwenda kukatwa mguu. Akenda akashuhudia pale wakalizana, mama kakatwa mguu haikutimia miezi mitatu kafa, kijana kabakia peke yake.

Lakini bahati nzuri kwa kijana huyu ilikuwa ndio leseni, ameacha madawa ya kulevya na sasa hivi mswalihina mkubwa na kila wakati akimkumbuka mama yake anasema mimi ndio niliyemuua mama yangu, anasikitika.

Mhe. Spika, kesi ya tatu niliyoishuhudia, kuna mzee mmoja aliweka shilingi zake laki mbili ndani, mwanawe anatumia madawa ya kulevya pesa kaziiba. Mzee huyu kachukua bakora kamkamata mwanawe kwa uchungu anampiga ghafla kadondoka, kabebwa kufika hospitali anaambiwa mzee mwanao amekufa.

Mhe. Spika, ya nne siku moja nilikwenda Mahakamani hapa kwa shughuli zangu binafsi, nilimkuta mama mmoja tena mkaazi wa jimbo hili hili la Kikwajuni, kakaa kwenye benchi analia, kwa bahati nilipopita akaniita "Mheshimiwa nisubiri", Nikamsubiri, ananambia nina mtoto wangu amekamatwa kwa kuiba yuko kitunduni kule. Mimi pale fikra zangu moja kwa moja zikanijia labda anataka nimsaidie atoke.

Lakini akanambia ninachoomba unisaidie huyu mtoto afungwe, kwa sababu kutokana na matatizo haya ya madawa ya kulevya yaliyoingia, ameshaniibia kila kitu! Hivi sasa anaiba kwengine, ninakuwa na wasi wasi huko sijui nitaletewa maiti, ama nitaletewa kishajeruhiwa vibaya sana, sasa bora afungwe ili mimi nipate afueni kidogo. Ananambia huku analia.

Mhe. Spika, nilimuonea huruma, nilikwenda kuuliza kesi yake iko kwa Jaji gani nikaipata, bahati Jaji hajaingia kwenye Mahakama yuko kwenye chumba chake, tena kile chumba ulichokuwa ukikaa wewe Mhe. Spika. Nikenda

nikazungumza na Jaji nikamwambia msikilize huyu mama kilio chake, akamsikiliza, Jaji akaagizia *file* likaletwa.

Akatumia hekima Jaji akamwambia unaona mama yako huyu na Mheshimiwa wamekuja kukuombea, hebu tuambie umeiba, hujaiba. “Aaa kweli nimeiba, lakini naomba unisamehe mimi sifanyi tena, *father* nisaidie”. Alipokubali tu Jaji akamfunga miaka miwili, akamwambia basi nakufunga utakwenda Chuo cha Mafunzo miaka miwili ili ukatulize akili yako.

Basi mama yule aliacha kulia akamshukuru Jaji, akanishukuru mimi, katoka pale na furaha. Mzee anataka mtoto wake afungwe ili apate afueni na anafurahi. Hapo ndio tulipofikia.

Mhe. Spika, si hiyo tu, kuna mama mmoja alianika nguo zake kanga mpaka chupi na vitu vyengine. Mtoto kaviiba vimaji kavitia ndani ya shati mle, kuna mzee mmoja kwa bahati kamuona wakati anatungua akamfukuza kwa mikwaju, yule mzee mzima kidogo. Kwa bahati huyu kijana katika kwenda yake mbio, kafukuzia mwenyewe Madema, kufika na mzee kenda huku anampiga bakora, nini, akamwambia kaiba vitu katia ndani ya shati, kutolewa nguo zile zimaji zimo ndani ya shati.

Yule kijana anasema Polisi kule “Huyu mzee chizi, kwani hivi vitu vyake nilivyoiba, hivi vitu vya *mother*,” kamuibia mama yake. Kuitwa mama yake, mama yake akasema aaa kishazoea kuniibia nipeni vitu vyangu basi mimi sitaki kesi. Yule mama wa mwanzo alikuwa jasiri kumfunga mwanawe, lakini huyu anasema mimi sitaki kesi nipewe vitu vyangu basi.

Mhe. Spika, ya sita niliyoshuhudia kuna kijana mmoja kapewa madawa akauze na yeye mtumiaji wa madawa, mengine kauza, mengine kameza mwenyewe, waliompa madawa wakawa wanamtafuta. Wamemtafuta hata siku hiyo wakaja wakamkuta maeneo ya Miembeni wakamzunguka watu wanne kila mmoja ana kisu, akaambiwa “Utatupa pesa zetu au tutakuua”. Kijana yule akawa anajitetea. “Mimi kweli bwana nimeuza mzigo lakini kwa bahati nilikamatwa na polisi pesa zote wamechukua polisi”. Wanamwambia muongo ungekamatwa na polisi tungepata taarifa, kwa kiasi walivyokuwa hodari maana yake angekamatwa wangepata taarifa. “Hujakamatwa muongo utatupa pesa zetu au tutakuua”.

Yakenda majadiliano, hatimaye wakamwambia wewe pesa za kutulipa huna sasa kubali tukukate kidole kimoja tukusamehe. Akasema nimekubali lakini nataka mnikate kidole hiki kidogo, wakamwambia hata tuchague wenyewe kidole cha kukata. Mmoja akasema tumkate kidole hicho cha kutolea shahada akitaka kusali pia ashindwe asiweze kutoa shahada. Mhe. Spika, wamemkata

hapa wameking'oa kabisa mpaka leo kabakia hivi vitatu na hiki kimoja, hiki hakimo.

Tena Mhe. Spika, kama ingelikuwa mimi na wewe tunakatwa kidole tungeanguka tukafa pale pale, lakini wala unga madhubuti! Kachukua kipande cha kidole chake mpaka hospitali kaweka ma-*tissue* tu hapa, kufika anakwenda anaomba hospitali asaidiwe kile kidole kiungwe. Akaambiwa kidole kimeshakufa hakiwezi kuungwa, wakamshona wakamtengeneza hapa yuko mitaani mpaka leo huko. Ndio nikasema Mhe. Spika, mswada huu umechelewa watu wameshapata hasara kubwa sana.

Lakini hasara nyengine kubwa siku moja kulikuwa kunatolewa mawaidha msikitini, akaja mla unga mmoja kasimama dirishani anasikiliza na bahati nzuri mawaidha yenyewe yalikuwa yanahusu ulevi. Kasikiliza watu ndani wanamtizama huyu maadam anasikiliza labda yatamwingia, basi alimaliza tu "Watishe, watishe, tustarehe peke yetu," kwamba imeshamuingia sasa ile anaona watu wanatishwa wao wapate kustarehe. Sasa hayo Mhe. Spika, ndio matatizo yaliyoingia. *(Kicheko)*

Mhe. Spika, kuna watu walioingia ufukara, kuna watu walioingia umaskini kutokana na mambo haya. Kuna mama mmoja alikuja akanisikitikia katika ujane wake alijitahidi kutafuta vyombo vya dhahabu ili mtoto wake akioa ama kuolewa aweze kuwapa zawadi. Matokeo yake mwanawe akaingia kwenye unga hana chochote, anasema kaingia ufukara kabisa.

Kuna wazee waliotegemea watoto wao wawazike sasa wazee ndio wanazika watoto. Kuna watoto waliofarakana na wazee wao hawatambuani, yote hii ni sababu ya madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, mtaa wa Miembeni wameanzisha pale Kitengo cha Kupambana na Madawa ya Kulevya kupitia Mradi wa *TASAF*, ni mradi wa UKIMWI, bahati nzuri mimi ndio mlezi wa kikundi kile. Hivi karibuni nikawaambia hebu waiteni hawa wateja wote tuje tukae tuzungumze nao. Nikatoa pesa nikawaambia kanunueni soda, maji tuwawekee hapa tuje tuzungumze nao. Nikamtafuta mteja mmoja ambaye ameacha pombe ili aje azungumze nao.

Mhe. Spika, kikao kilikuwa kizuri walikuja wengi tukazungumza nao. Yule mteja aliyewaambia jamani nyinyi si mnanijua mimi nilikuwa mwenzenu huko, nikaachana na mke wangu, watoto wangu nikawa siwajui kutwa niko kwenye unga tu, nimekubali kuacha , nimeacha hivi sasa nimepata kazi, asubuhi nafanya kazi na usiku nafanya kazi ya *watchman*. Nimerudiana na mke wangu na watoto wangu ninao pamoja sasa hivi, ninaswali na bahati nzuri msikitini

sasa hivi nimepewa nafasi ya kuadhini. Hamuoni kiasi mafanikio niliyopata hebu acheni, akazungumza nao vizuri.

Mhe. Spika, nikapata nafasi mimi ya kuzungumza nikazungumza nao, katika kuzungumza yangu mwisho nikawaambia jamani eee hebu tazameni hali yenu mlivyo. Hilo dengrizi lako limeshachanika chini lote, wewe kutwa unahangaika kwenda pwani huko, uende masokoni huko uchomoe, unyang'anyee, ubebe mzigo upate pesa unahangaika.

Lakini pesa zako zote unazopata unakwenda kumpa muuzaji wa unga. Hebu mtazameni yule anayekuuzieni, ana nyumba nzuri, ana gari mbili nzuri, kaoa mke mzuri, kwa nini mnamtajirisha yule. Hizi pesa mnazopata nyinyi katika mambo yenu hayo hayo hata kama ya kuiba kwa nini msile vizuri mkajitengenezea maisha yenu. "Kweli *father,* kweli, unatwambia kweli, tusomee duaa". Haya.

Mhe. Spika, kikao tumemaliza kama saa kumi na mbili nimerudi nyumbani nakwenda kwa mdogo wangu nikapita njia za vichochoroni. Wale walionambia *father* tusomee dua nimewakuta nyuma uchochoroni kuna baraza Mhe. Spika, wameshusha suruali mpaka hapa, huko kwenye bamkubwa mwenyewe ndiko kunakopigwa sindano (sehemu ya siri). Mhe. Spika, nilitetemeka na kuogopa na mwisho nikikwenda mbio. Kwa kweli wenyewe wanasema "*father* usiogope," nilisema hapa hapakaliki. Hali hiyo ndiyo tuliyofikia Mhe. Spika *(Kicheko/Makofi).*

Kwa hivyo, napenda kumuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kuhusu kile kitengo ambacho ametuambia anataka kukijenga Tunguu kwa kushirikiana na *ZAYADESA*, basi ajitahidi tukijenge haraka. Kwa sababu nilipowasomea vijana wale wanataka kuacha na ndio mama walisema kwamba *father* tusomee dua, lakini *micotine* imeshawaingia mpaka ndani ya damu yao, hivyo hawawezi kuacha kama hawakupata kitu cha kuweza kuwasaidia.

Kwa maana hiyo, Mhe. Waziri ajitahidi sana hiki kitengo kijengwe kwa haraka, ili kiweze kuwasaidia hawa vijana, kwa sababu hali ni mbaya sana huko Ng'ambo na wala sio Miembeni tu, yaani shehia zote mambo yako hivyo.

Mhe. Spika, katika mswada huu nimeona masuala ya Jeshi la Polisi yamo. Lakini nina wasiwasi sana na Jeshi hili, kama tutawaachia kazi hii sijui kama kweli itakwenda. Kwa sababu siogopi kusema kwamba Polisi sasa rushwa ndiko ilikohamia na nitatoa ushahidi. Mhe. Spika, mimi niliwahi kuwa sheha tuliwahi kwenda kusachi si mara moja wa mbili na kukamata huu unga, lakini ajabu huyu mtu anakamatwa na ikifika jioni unamkuta tena yupo Miembeni, ukimuuliza vipi? anakwambia askari wenyewe si njaa tupu! Hali hii

inamaanisha nini? Kwamba ametoa chochote na ameachiwa, ndio maana ya njaa.

Wakati nilipokuwa nikikaimu Mkoa wa Mjini Magharib alipokuwa Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib akiumwa, *ZRB* walipata agizo kwamba katika Mkoa wa Mjini Magharib kunatokezea wastani wa ajali tatu kwa kila siku. Sasa agizo ni kwamba madereva wazembe wote wanyang'anywe leseni, suala lile *ZRB* ikabidi waishirikishe na Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini, kwa ajili ya kuangalia kitu gani cha kufanya. Kwa hivyo, tulikubaliana tufanye kikao cha *ZRB*, *TRA*, Afisi ya Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Kitengo cha Usalama Barabarani, Wapasishaji wa Vyombo vya Moto, ili kwa pamoja tuangalie nini cha kuweza kufanya kupunguza hizi ajali.

Lakini swali lilikuja Mhe. Spika, kwenye *traffic* kila siku si wako njiani, haya matatizo hawayaoni? Sasa tukifanya operesheni hii tukiwaachia *traffic* tutafanikiwa? Tukasema hatufanikiwi. Tufanye nini? Maafisa wa *ZRB* washirikishwe, kila *traffic* wanne tuweke mmoja wa *ZRB* na tusitangaze. Siku tunayoamua kufanya operesheni tuwaite asubuhi, mchana ianze operesheni.

Mhe. Spika, tukaweka siku ya Ijumaa asubuhi saa 4:00 *Traffic*, kwa ajili ya kuzungumza nao kwamba tunataka operesheni hii na ianze baada ya Sala ya Ijumaa. Kwa kweli polisi walisema aa bora operesheni hii ianze Jumatatu, maana yake Ijumaa siku ndogo, viongozi wanakwenda kusali inabidi tuwalinde, yaani maeneo mengi, basi mimi na Kamishna wa *ZRB* tukawa tunatizama tu, kwa sababu walikuwa wanatafuta njia, ili waende wakasema. Mhe. Spika, tuliwaambia hapa lazima ianze leo na kila kwenye askari wa nne wa *Traffic* atakuwepo afisa wa *ZRB* mmoja.

Kwa hivyo, tulikwenda operesheni tuliyofanya kwa wiki tatu basi serikali imeweze kukusanya zaidi ya shilingi milioni 500. Sasa suala la kujiuliza hawa *Traffic* wapo njia siku zote haya makosa hawayaoni mpaka tufanye operesheni maalum. Kutokana na hali hiyo, naona utendaji wa polisi hauko makini katika suala hili.

Mhe. Spika, pia kwenye mahakama zetu kuna haja ya kuziangalia, kweli kesi 47 au 48 zinakwenda zote zifutwe. Kwa mfano, kwenye Mahakama kuna masuala ya hekima za Mahakimu, kwa sababu Mhe. Spika ulikuwa Hakimu lakini hukutumia hekima hizo. Kuna mtu wa alikamatwa analo shamba la bangi Saateni, sehemu ya kufulia nguo zamani (Dobi), baada ya kupelekwa mahakamani alihukumiwa kifungu cha mwaka mmoja na nusu.

Kwa kweli mtu yule hakuridhika na alikata rufaa Mahakama Kuu, basi Mahakama Kuu ilimfunga miaka 15. Baada ya hapo alikata tena rufaa katika

Mahakama ya Rufaa na Mahakama ya Rufaa ilimuachia huru na ilisema ameonewa, kwa sababu sheria inasema kesi ya bangi mwisho ni miaka mitano na huyu amefungwa miaka 15, kwa hiyo mahakama ikamuachia.

Mhe. Spika, tunaona hekima hiyo maana unajua kifungo chake ni miaka mitano na unamfunga miaka 15, ili huku ajekutoka. Sasa haya ndiyo matatizo ambayo tunayo.

Mimi sifikirii Mkemia Mkuu kama atapelekewa *Cocaine and Heroin* aseme kwamba hii saruji au sembe ama jivu! Kwa sababu yeye anasema kile ambacho amepelekewa. Isipokuwa ushahidi unapotezwa huku kunakokamatwa na huo ndio ukweli na kama tutategemea polisi haitofanya kazilekewa.

Ushauri wangu Mhe. Spika, tuunde kitengo maalum, yaani kuwe na askari maalum haidhuru tuchukue askari kutoka Jeshi la Polisi, Kikosi cha KMKM, JKU pamoja na Valantia tukuwakusanye pamoja na tuseme sasa hiki ni kikosi cha kupambana na madawa ya kulevya, nadhani hiyo inaweza ikasaidia sana. Kwa kweli kama hatutakuwa na kikosi maalum tukawatafutia na zana pamoja na hao mbwa basi hatuwezi kufanikiwa, yaani mswada huu hautofanyakazi.

Kwa hivyo, lazima tuunde kitengo maalum cha kupambana na madawa ya kulevya. Kwa sababu hivi sasa kitengo hiki wanacho Jeshi la Polisi na huwa wanakuja sio kama mbwa wote wamekufa, wao na wanakuja nao pale Miembeni huwa nikiwao. Lakini wanapokuwa kwa ajili ya kuchukua fedha tu.

Mhe. Spika, jana Mhe. Aziza Nabahan Suleiman alisema kwa uchungu ni kweli, nyumba zinazouzwa dawa za kulevya utaona madirisha yake wametia ule wanya wa kashata, lakini kuna sehemu ndogo chini ya kupitisha vidole viwili. Kwa hivyo, kinachofanyika mtu kukamata fedha zake na yule muuzaji anachukua dawa na kupenyeza, yaani hivyo ndivyo zinavyouzwa.

Sasa ninashauri sana haya masuala tusiyafanyie mzaha, isipokuwa tuende nayo kikweli kweli kwa kuwa na kitengo maalum ambacho kitakuwa na askari maalum watakaoshughulikia madawa ya kulevya *(Makofi)*.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumze mambo ambayo Waheshimiwa Wajumbe wengi wamezungumzia kuhusu Kamati ya Mawaziri. Mhe. Spika, nilikuwa nikijuiliza imeundwa au inapendekezwa kuundwa Kamati hii ya Mawaziri kwani huku wizarani ndiko kunakouzwa unga. Mhe. Spika, unga haiuzi wizara, isipokuwa unga upo mitaani, yaani kwenye shehia zetu, wilayani pamoja na mikoani.

Sasa ushauri wangu hapa pamoja na kuwa hii kamati ya kitaifa ambayo imeshirikisha mawaziri wote, basi ni vyema ingefanywa ikawa ndogo. Lakini tukawa na kamati kuanzia shehia huko kunakouzwa unga wenyewe, tuwe na kamati katika wilayam, shehia wanapeleka kwenye wilaya na wanafanya uchunguzi, unakwenda mkoa na kuangalia kwa pamoja na halafu sisi ndio tunapeleka taarifa kwenye kamati kubwa.

Kwa hivyo, nadhani hali hiyo ndio inayoweza kutusaidia kuliko kuwa na kamati moja tu ya mawaziri wakati unga unauzwa huko vichochoroni, itakuwa haifanyikazi. Mhe. Spika, ni vyema kuwa na kamati kuanzia shehia na tukipata watu wazuri, kweli kwenye shehia wako watu wazuri ambao wanaweza kutusaidia.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib aliwakusanya wazee wenyewe watoto wote walioathirika na madawa ya kulevya, kwa sababu wanayo kamati yao ya wazee. Mhe. Spika, wazee wale wanauchungu sana kuona watoto wao namna wanavyoteseka. Sasa wazee kama wale wakiwemo kwenye kamati ndio watakaosaidia sana, lakini mawaziri tu iwe kamati hii, bado hatujafanya kitu hapo.

Mhe. Spika, nashauri sana kamati hizi zianze kwenye shehia, wilaya, mkoa na halafu kuwe na ile ya kitaifa. Nadhani tukifanya hivyo naamini kabisa taarifa tutazipata vizuri sana. Lakini taarifa zake hizi kuanzia shehia kuwe na kitengo maalum cha kupeleka na wala isiwe polisi. Kwa sababu hivi sasa tunayo Polisi Jamii na tunawashawishi watu wengi sana wajiunge kwenye Polisi Jamii.

Kwa mfano, Paje hivi sasa utakapokwenda Mhe. Spika, tumeweza kutuliza hali zote, yaani machafu yote tumeweza kuyadhibiti pale. Lakini bado watu hawaamini polisi wanasema unapopeleka kesi yako polisi, yaani ukiwapa taarifa polisi unawapelekea kula. Sasa kukiwa na kitengo maalum ambacho kitakuwa kinashughulika na mambo haya na taarifa tukawa tunazipeleka kule na wao ndio watakazishughulikia, basi hapo ndipo tunaweza kufanikiwa kwenye mswada huu, vyenginevyo tutakuwa tunakata mbayaya hata mbuzi hali.

Mhe. Spika, kifungu cha 15 cha mswada huu kinaruhusu serikali kufanya ukulima wa mchanganyiko wa madawa ya kulevya na pia inaruhusu kusafirisha nje. Hivyo, wasi wasi wangu tunafahamu kwamba tupo wajanja wengi, tunajua haya madawa yanatumika katika kutibu binadamu na lazima yanahitajika kuna *pharmacy* zinauza hizi dawa. Mimi nakumbuka kuna *pharmacy* moja ilifungwa kwa sababu ya kuuza dawa hizi.

Mhe. Spika, kama tunaruhusu kama mswada ulivyosema huu ukulima wa mikoko na mambo mengine tutaudhibiti vipi kwani badala ya kutoka nje sasa itakuwa tunaruhusu watu walime humu humu. Mhe. Spika, hili naomba tuliangalie vizuri lisije likatuletea matatizo. Maana ukiruhusu watu kulima ama serikali ilime kwa matumizi watu wanaweza wakaitumia fursa hiyo vibaya ikaja ikatuadhibu huko mbele tunakokwenda. Kwa hivyo, udhibiti wake Mhe. Waziri sijui utakuwa vipi.

Mhe. Spika, pia haya madawa kwa kuwa yanatumika kama matumizi ya madawa kwa binadamu baadhi ya maradhi, huku hospitali sijui udhibiti wake uko vipi. Mimi naona haya mambo si madogo kwa kweli yanataka mtu atulie, tuwe na mshikamano mzuri na tuseme sasa tunataka kupiga vita mambo haya.

Mhe. Spika, nimesema inawezekana kwa sababu katika miaka ya 80 alisema Mhe. Aziza Nabahan Suleiman kwamba palizuka wimbi la kuibiwa televisheni ambazo zilikuwa zinasafirishwa. Mhe. Spika, ilichofanya serikali wakati ule ni kwamba watafutwe hawa wanaosafirisha ili wawekwe ndani. Walipokamatwa wakaekwa ndani wote basi wizi ulitoweka na watu wale hawakutoka mpaka alipobadilika Rais baada ya kuondoka Mzee Aboud Jumbe Mwinyi alikuja Mzee Ali Hassan Mwinyi ndio wakatoka. Lakini wizi wa televisheni wote uliondoka, ndio nikasema kama tutakuwa makini tukasema sasa hebu tufanye hii kazi ya kudhibiti basi suala hili linawezekana. Mhe. Spika, lakini lazima mashirikiano ya watu wote yawepo, watu wasiogope wawe wa kweli, washiriki kikamilifu hili suala linawezekana.

Mhe. Spika, baada ya mchango wangu huo mdogo naunga mkono mswada huu na nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote kwa sababu mswada huu unamgusa kila mmoja wetu Mhe. Kamal Basha Pandu kama hakusema basi hakuwafanyia haki wananchi wake kwa sababu Mlandege yamejaa tele. Mhe. Waziri Kiongozi nae kama hakusema basi hawafanyii haki wananchi wake kwa sababu Mwanakwerekwe umejaa tele. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Ali Moh'd Bakari: Mhe. Spika, kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataala kwa kutuwezesha kufikia sasa hivi tukiwa bado tuko hai. Pia nikushukuru na wewe kwa kunipatia fursa angalau kwa uchache na mimi nitoe mawazo yangu juu ya mswada huu ambao sasa hivi unajadiliwa.

Mhe. Spika, huu mswada ni mswada muhimu sana kujadiliwa na kuletwa hapa, lakini mimi nilitaka nianzie pale alipomalizia msemaji ambaye sasa hivi amekaa kwamba mashirikiano yanahitajika juu ya kupambana na kadhia hii ambayo tuko nayo. Mhe. Spika, ni kweli mashirikiano ya kila hali yanahitajika, lakini mashirikiano yatapatikana pale ambapo watu watakuwa wanaelewana

vizuri na wakiwa watu wanaelewana vizuri ndipo mashirikiano yatakuwa yanapatikana. Mhe. Spika, sasa hivi katika nchi yetu tunavuta sasa hapa kimsingi hatuwezi kupata mashirikiano ya moja kwa moja katika kupambana na janga hili. Ndio maana nasema mashirikiano yanahitajika kwa sababu ya umuhimu wa sheria hizi tunazowatungia wananchi, kwa sababu wanaohukumiwa ni viumbe, basi kungekuwa kuna haja ya kutafuta uwezekano wowote ili tukapata mashirikiano ya moja kwa moja, ili tukija hapa katika Baraza letu tukufu basi kila mmoja akapata kuchangia na kila mmoja akapata kuunga mkono juu ya kile anachokiona kwamba anastahiki kukiunga mkono au anastahili kukipinga.

Mhe. Spika, hapa tumejadili miswada mwisho wewe unasema nani anayekubali na nani asiyekubali. Wale wanaokubali wananyanyua mikono na wanaokataa tunakaa kimya. Kwa hivyo, kama tunaokataa tunakaa maana yake bado kimantiki hatujazipitisha sheria inavyotakiwa kwa sababu hapa kinachoonekana ni kwamba hata mmoja tu akizidi katika wale ambao wamekataa basi itakuwa hii sheria imeshapita.

Mhe. Spika, mimi nilidhani kama tungekuwa na maelewano ya kweli kweli kambi zote mbili, labda huko wangelitokea wawili au watatu wakapinga na huku wangetokea kama hao wakapinga lakini walio wengi ndani ya Baraza hili wakawa wameiipitisha. Mimi nadhani hapo sheria hiyo ingekuwa imefanyiwa kazi katika muundo wa kujenga mazingira ya hali halisi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, lakini katika hali hii tuliyonayo sasa hivi mimi naona kama bado tutafute maelewano ya kweli kweli ili kusudi tuweze kuwatendea haki wananchi wetu. Kwa sababu sasa hivi kwa mivutano hii tuliyonayo, mimi sidhani kama tutapata mashirikiano ambayo hapa yametajwa.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba haya madawa ya kulevya yanaathiri jamii zetu na sasa yanaathiri ulimwengu mzima kwa sababu kila pahali haya huvutwa na wengine wanapanda huko. Hapa kwetu sina hakika kama hapa petu mimea hii inamea ukiacha bangi. Mhe. Spika, ni kwamba kinachochangia ni kuwa mashirikiano ya moja kwa moja yapatikane na kulifanya jambo hili au maovu haya yaendelee kutanda katika nchi hii kwanza ni namna ya vyombo hivi vya ulinzi vinavyofanya kazi zake na vilivyokuwa havitoi mashirikiano ya moja kwa moja na wananchi juu ya suala hili la madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, askari wote wanajua maeneo yote yanayovutwa bangi na wanajua maeneo mengi yanamouzwa haya madawa ya kulevya. Mhe. Spika, nataka nitoe mfano ni kwamba maeneo ya karibu ninamoishi mimi kule Bububu Mshelishelini kuna eneo moja nimeshawahi kulisemea katika Baraza hili kwamba kuna eneo pale linauzwa bangi na gongo tena wanatoa benchi pale nje

maana yake hawafanyi siri. Juzi usiku mimi nilipita pale nilikuwa narudi kumpeleka jamaa hospitali nikachelewa nilikuta vijana wa kike na wakiume wanavuta bangi na wengine wanakunywa gongo. Mimi niliwauliza vipi vijana salama wakaniambia mzuka tu huu. Mhe. Spika, nikaona hizi lugha wanazozungumza za kibangi bangi halafu ndio zinakuwa kauli zinazozungumzwa humu mitaani.

Mhe. Spika, pale askari wote wanapaona lakini unapokwenda kutoa taarifa wakija wakiwakamata wale basi siku ya pili tu unawakuta wale vijana wako mitaani. Kwa hivyo, hapa kinachofanyika ni nini, ni hasama baina ya yule aliyekamatwa na yule aliyesema. Kwa sababu askari mwisho wanawaambia ni fulani na fulani ndiye aliyekuja kutwambia hapa. Kwa hivyo, mimi naona hapa mashirikiano hayawezi kupatikana kwa sababu watu wanaona kwa hali hii hivi vitendo wacha viendelee kufanyika kwa sababu sisi tunasema halafu hawa ni wahuni wanakuja kutuchomea nyumba zetu moto.

Mhe. Spika, hata wengelikuwa hawawaambii mtu ukishamkamata na bangi anaivuta halafu wewe unahitaji ushahidi, ushahidi huo wa nini na kama unahukumu hukumu tu. Mhe. Spika, kwa sababu kuna matukio mengine sio ya kudhania, matokeo ambayo yanahitaji msororo mrefu na wewe ukaingizwa katika mkumbo. Kwa hivyo, hapo Mahakama inapasa kuchunguza na kuangalia lakini mimi ukishanikamata na bangi navuta halafu unanipeleka Mahakamani, Mahakama inasema inatafuta ushahidi siku ya pili Hakimu anaona kama mimi sina hatia. Mhe. Spika, hatia ingekuwa ni ipi wakati ile bangi nimekamatwa nayo.

Mhe. Spika, kuna makosa makubwa makubwa yanayohusiana na makosa mbali mbali lakini mtu akikamatwa na ndizi changa kwa sababu ya njaa yake basi anafungwa miezi sita mpaka nane. Kwa hivyo, tunaona kwamba tutafika pahali maamuzi yanayotolewa Mahakamani yanavunja moyo kwa sababu watu waliokuwa na makosa makubwa wanaachiwa na hatimae yule aliyefanya kosa dogo tu wakati mwengine kwa njaa anakamatwa na kufungwa. Kwa hivyo, mimi naona hayo yanavunja moyo.

Mhe. Spika, mimi nadhani ipo haja ya kuangalia ni namna gani ya kusimamia hizi sheria zetu kwa sababu tusipokuwa tunazisimamia sheria hizi basi itakuwa kila siku tunakuja humu tukipanga mwisho tutaonekana machale. Kwa sababu tunakuja tukisimamia mambo halafu hatuyasimamii na yakishasimamiwa wanatafutwa wale wanyonge wanaonewa wale wenye uwezo wanatoka.

Mhe. Spika, ukiangalia suala la madawa ya kulevya watu wengi wanaoyaleta hapa nchini wanajulikana, lakini kwa sababu wana uwezo na nguvu za aina fulani, basi utakuta kwamba halafu wanaachiwa hawachukuliwi hatua yoyote

anakuja kukamatwa mtu aliyekuwa na kete moja. Kwa hivyo, sisi tunakuwa tunafanya biashara na watu hawa halafu tunawalinda matokeo yake madawa yanaingizwa nchini na baadae hakuna hatua yoyote. Mhe. Spika, hakuna anayeleta madawa isipokuwa ni sisi wenyewe hapa hapa na tunajuana.

Mhe. Spika, mimi nafikiri kwa sasa kutokana na hali ilivyo pamoja na sheria hizi na adhabu zake ambazo hapa zimetajwa, lakini ipo haja kubwa sana ya kudhibiti madawa haya ya kulevya kwa njia hizi za anga na bandari. Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano hapa kwamba ipo haja katika kamati hii ambayo imeundwa hapa ya Baraza la Mawaziri na Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi angekuwemo kwani ni mtu muhimu sana kuwemo katika mswada huu kwani tunatafuta namna ya udhibiti.

Mhe. Spika, licha ya kwamba mawaziri waliotajwa hapa kwamba wataingia, hapa mawaziri wakiweza basi itakuwa tumefanikiwa, lakini wakikosa kufanikiwa basi wataonekana na wao wamo. Kwa hivyo, mimi naona hii tume iliyoundwa kuwepo kwake wangelitafutwa watu wengine wasiokuwa mawaziri wakaunda hii tume halafu wakasimamia kazi hii kwani hii kazi haina uzuri, hii kazi itakuwa ni nzuri pale mawaziri watakapoweza kudhibiti. Lakini wakikosa kudhibiti hali hii na madawa yakawa yanaingizwa na watu wanavuta basi na hawa mawaziri na wao watakuwa wamo kwa nini wasidhibiti na wameunda tume hii kwamba wadhibiti janga hili.

Mhe. Spika, tafsiri katika jamii zitakuja nyingi na mbali mbali na kila mtu atasema vile anavyoona. Mimi naona katika uundwaji wa tume hii kungekuwa na mabadiliko kidogo ingawa hapa imeshapitishwa lakini mimi naona Mhe. Waziri angeliwatafuta watu wengine maarufu ambao wanaweza kuifanya kazi hii kwa mafanikio zaidi. Mhe. Spika, mimi naona hapa waziri kwa cheo chake hastahili kabisa kuingia katika chombo hiki wakawa wanashirikiana na wavuta bangi na waingizaji wa madawa ya kulevya. Mimi naona mimi nipo pamoja na Mhe. Hija Hassan Hija tuingizeni sisi tufanye hizi kazi, sio kuchukua mawaziri wafanye kazi hii.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naona tutafute utaratibu mwengine zaidi wa kulikabili tatizo hili kwani jamii yetu itaathirika sana na madawa haya ya kulevya. Mhe. Spika, watu hawa wanaotumia madawa haya wapo wengi sana na hawa ni nguvu kazi ya taifa tunawahitaji hawa. Mhe. Spika, pamoja na yote ambayo yamezungumzwa na michango mbali mbali ambayo mawaziri wametoa, lakini lazima na vyombo vinavyohusiana na kutoa haki visimamie hili ili kusudi tutoe fundisho katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba ikiwa atabainika mtu ameshakamatwa na madawa ya kulevya lakini akatokea ndugu yake au jamaa yake kwenda kumchukulia dhamana ina maana yeye ndiye aliyemtuma. Anachotaka kukifanya ni kuchukua dhamana ili atoke halafu afanye maarifa ya kuwa mtu huru. Mhe. Spika, mimi nasema watu wa aina hii licha ya kwamba dhamana ni haki ya mshitakiwa, lakini kuna makosa mengine kwa ubaya wake tu hayastahili mtu kupata dhamana ya haraka haraka.

Kwa hivyo, kwa makosa haya ya madawa ya kulevya basi kama mtu anakatwa nayo dhamana yake kidogo iwe na ugumu ili wale wanaotumwa wasiwe tayari kwenda kuyachukua kwa sababu wanaotumwa ni watu wanyonge tu. Lakini wale wanaotuma ni matajiri ambao wamekaa wanajua kwamba akikamatwa mtu wake ni vipi atamtoa atatumia njia zake zote anazozijua na uwezo wake kwa sababu wanakuwa na kiapo chao kwamba mimi nakwenda huku lakini nikikamatwa unitoe.

Kwa hivyo, mtu hukubali hicho kiapo chao halafu anapelekwa mtu na ndio maana watu wengi wanaokwenda huko wengi hatima yake wanakuwa nje. Kwa hivyo, na hawa wanaowatuma licha ya kwamba jamii imeshataja mazingira yatakayowashika lakini na hao wanaowachukulia dhamana na wao ibainike kwamba na wao wamewatuma. Mhe. Spika, mimi naona na hawa nao wangeliandaliwa utaratibu wa kuonekana kama na wao ni wahusika wakubwa sana juu ya kuwepo balaa hili.

Mhe. Spika, tukija katika utoaji wa sheria mara nyingi jamaa zetu hawa nao wana mashaka yao katika kusimamia hukumu hizi. Ukija katika vyombo vyetu hivi mtu tayari ameshakamatwa na unga lakini anaandaliwa mazingira mazuri anaambiwa wewe usiwe na wasi wasi mimi nitakuletea chakula, lakini baada ya muda fulani mimi nitakuachilia ili tuangalie mazingira mengine. Mtu kama alikuwa anastahili kufungwa miaka 15 halafu anakuja kuambiwa bwana ulikuwa ufungwe miaka 15 lakini kwa sababu bosi ameshatoa kitu kidogo ataambiwa wewe itabidi uende mwaka 1. Kwa hivyo, badala ya kuzuia na kutaka kudhibiti badala yake tunaendeleza kwa sababu mwaka kila mtu anaweza kwenda madhali ni kazi yake. Mhe. Spika, mimi nadhani tusipoangalia mambo haya basi yatatuathiri kiasi kwamba kila baada tunayokwenda nayo nguvu kazi ya taifa itapotea itafika wakati nchi yote itakuwa imetawaliwa na wavuta bangi.

Mhe. Spika, lililo kubwa zaidi mimi nadhani uingiaji wa wageni katika nchi yetu kwa hisia yangu mimi naona na wao wamechangia kwa kiasi kikubwa zaidi. Kwa sababu balaa nyingi katika visiwa hivi vya Unguja na Pemba hazikuwepo wala hazikuwa na urithi kwa sababu hao wazee wetu huko nyuma walikuwa hawafanyi mambo haya. Kwa hivyo, mambo mengi hayakurithiwa

hapa Zanzibar ambayo yamekuja, lakini yamerithiwa kutokana na uingiaji wa wageni katika visiwa vyetu.

Mhe. Spika, leo watu wanakuja katika nchi yetu kama wanaokwenda pwani maana yake hawaulizwi kila anayekuja hapa yeye ni Mzanzibari tu. Kwa hivyo, hata mtu awe anatoka wapi ukimuacha mzungu kwa sababu ya rangi yake lakini mtu mwengine yeyote anakuja na marasta mpaka miguuni wala haulizwi anapotoka. Mhe. Spika, kwa kweli na hili nalo ni tatizo na linachangia uingiaji wa madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, kama hatujaweza kudhibiti jambo kubwa la uingiaji wa watu Zanzibar bado tutakuwa hatuwezi kuzuia madawa ya kulevya hata siku moja hata tukafanya kitu gani. Kwa hivyo, Baraza la Mawaziri na waunde kamati yao mwisho watakuja kujiona wanachezea mbwa na wao watawaacha. Mhe. Spika, lakini ikiwa hatujaweza kudhibiti uingiaji wa wageni katika visiwa hivi suala hili litaendelea kuwepo na kila siku kuongezeka. Kwa hivyo, tusifanye jambo la tatu tukaacha la kwanza, hebu tufanyeni hili la kwanza tuandae utaratibu wa uingiaji wa watu katika visiwa vyetu, visiwa hivi ni vidogo mno wakiingia watu kidogo tu wanatuathiri.

Mhe. Spika, kuna bandari nyingi watu wanaingia kwa madau yanatoka Mombasa, Dar es Salaam wanakuja na madau na humu mote mnajulikana. Mhe. Spika, mimi nasema tuandae utaratibu wa uingiaji wa wageni katika nchi yetu kama tunataka kuzuia baadhi ya balaa hizi. Leo hapa Zanzibar imefika wakati kila kinachofanyika Tanzania Bara na hapa kinafanyika, hakuna tena nidhamu wala hakuna tena chochote wala hatuwezi kukaa tukaringa tukasema sasa Zanzibar ni nje atakae aje. Mhe. Spika, Zanzibar imekuwa ni nchi ambayo ina mabalaa mengi ambayo yanasababishwa na wageni. Mhe. Spika, kwa silka zetu hatukuwa hapa tulipo leo lakini kwa sababu ya matokeo mbali mbali ya kutokumudu uingiaji wa watu tukawafanya ni ndugu zetu matokeo yake wametuingizia balaa.

Mhe. Spika, mimi namshauri Mhe. Waziri katika hali hii kwa nia yake safi yakutaka kuzuia janga hili kubwa, baya na ovu kabisa ni vyema kuangalia tena upya namna gani tutadhibiti viwanja, tutadhibiti bandari, na tutatafuta watu gani maarufu ambao watasaidia. Mhe. Spika, mimi sikubaliani hata kidogo kwamba mawaziri na hii kamati yao waliyoitaja hii kwamba ndio isimamie suala hili, mimi naona hawataweza kabisa. Mhe. Spika, sikubaliani kwa sababu ukishajishabihisha na jambo basi lile jambo mara nyingi utaambiwa na wewe umo na utakuwa huna majibu mbele ya watu ukiambiwa na wewe umo. Mhe. Spika, kama kweli tunataka kudhibiti uingiaji wa madawa ya kulevya nchini na matumizi yake ni muhimu kwanza tuwe na mashirikiano ya kweli kweli katika

visiwa vyetu kwa sababu kila mmoja ana jukumu na ana wajibu wa kuzuia jambo ambalo ni baya katika visiwa hivi.

Mhe. Spika, ni kwamba tuelewane sisi wenyewe kwanza tukabiliane na mambo yetu kwa muda wetu. Lakini ni vyema kutafuta watu wa hizi kamati wa kuweza kuzikabili pamoja na watu wengine. Mhe. Spika, kama itawezwa kufanya kazi nzuri katika polisi jamii zetu basi hawa ni watu wazuri sana kuweza kuzuia kwa kiasi kikubwa kwa sababu wao maeneo yao wanayoishi wanajua bangi inapatikana wapi na unga unapatikana wapi. Nadhani tukiwatumia watu hawa vizuri basi kwa kiasi kikubwa mno hili tunaweza kupambana nalo, hata kama hatukuliondoa moja kwa moja kwa sababu mwanadamu na yeye ana hila yakuweza kufanya jambo lake lolote analotaka kulifanya. Kwa hivyo, tutaweza kuwahofisha watu ambao wanatumia madawa ya kulevya ikiwa polisi jamii hizi tutazitumia vizuri, tutaziwezesha kwa kweli zimeundwa polisi jamii maeneo mbali mbali nimeona mafanikio yaliyopatikana.

Mhe. Spika, kama kweli tunataka kuondoa janga hili la madawa ya kulevya mimi nadhani Mhe. Waziri atafute namna yakuunda polisi jamii katika maeneo yetu tunayoishi hasa maeneo ya mjini na maeneo ya kanda za pwani hasa huko mahotelini kila siku watakamatwa watu ili tuweze kukabiliana na wimbi hili. Pia Mhe. Spika, tuhakikisha kuwe na vyombo vyengine vya ulinzi ambavyo wale wataweza kuhofiana kuweza kurubuniwa na kufanya vitu vyengine ambavyo si haki kuvifanya.

Mhe. Spika, mimi sina mchango mkubwa sana juu ya mswada huu lakini muhimu ni maelewano ya pamoja ili tuweze kufikia hapa. Lakini ikiwa tutaweza kudhibiti masuala ya passpoti na uingiaji wa wageni pia hizi zinaweza zikatusaidia kwa sababu kuna siku pale Uhamiaji wakichacha wale watu wa bandari ndio wanapokamatwa siku nyengine huwa wanapita bila ya kuangaliwa. Mhe. Spika, unajua siku ambazo hawaangaliwi inawezekana ndio siku ile ile watu wanapopitisha hayo madawa yao tena kwa wingi. Mimi nasema kuna haja ya kusimamia udhibiti wa aina hii.

Mhe. Spika, nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba hata pale bandarini lile ni eneo kubwa sana linaloingizwa bangi, wale wanaochukua makaa wanachukua makaa huwa wanaingiza mifuko ya bangi tele huko halafu wanaingiza kwenye gari wanaondoka. Kwa hivyo, na humo ni sehemu za kudhibitiwa wakati mwengine kufanyike sanyi maalum ya maeneo hayo halafu tuone tumefanikiwa vipi katika hili. Mhe. Spika, kwa hivyo mule ni mwahali maarufu mnamotumika uingizaji wa bangi na madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, nataka niishie hapa ili niache utaratibu mwengine uendelee. Ahsante sana Mhe. Spika.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizoulizwa na Waheshimiwa wa Baraza lako tukufu.

Kwanza napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa wote waliochangia katika mswada huu. Michango yao yote ni mizuri na ya uhakika kabisa, yote tunaithamini.

Mhe. Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati yako ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa michango yao mizuri, mapendekezo yao mazuri waliyoyatoa kwenye kamati. Takriban michango na masuala yote ya Waheshimiwa wa Baraza lako tukufu yamezingatiwa na yamejibiwa na kamati hiyo, kwani kwangu mimi leo imekuwa ni urahisi sana kutoa ufafanuzi.

Baada ya hayo Mhe. Spika, sasa naomba kuwataja Waheshimiwa wote waliochangia. Waheshimiwa wote waliochangia ni 18 , ambapo wa kumi na nane yeye kachangia kwa maandishi.

1. Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii)
2. Mhe. Rashid Seif Suleiman (Waziri Kivuli Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii)
3. Mhe. Salmin Awadha Salmin
4. Mhe. Aziza Nabahan Suleiman
5. Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira
6. Mhe. Ali Denge Makame
7. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
8. Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi
9. Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi
10. Mhe. Ame Mati Wadi
11. Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi
12. Mhe. Ali Abdalla Ali
13. Mhe. Zakiya Omar Juma

14. Mhe. Ashura Abeid Faraji
16. Mhe. Hija Hassan Hija
17. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja
18. Mhe. Ali Moh'd Bakari
19. Mhe. Zahra Ali Hamad aliyechangia kwa maandishi.

Mhe. Spika, sasa kwa ruhusa yako naomba nizungumze kwa ufupi sana Mheshimiwa mmoja mmoja aliyechangia. Mhe. Ali Suleimani Ali yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii na pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani. Ametupa pongezi na pongezi zake zote tumezipokea na alitaka marekebisho ya mswada huu yafanywe ili kwamba kifungo cha maisha kiwekwe. Hii mheshimiwa alitaka madhumuni yake kuwa suala hili likome kabisa hapa nchini.

Kwa ufupi Mhe. Spika, sisi ndivyo tulivyopendekeza lakini kamati hiyo hiyo ambayo yeye ni Mwenyekiti, imependekeza kwamba isiopungua miaka 30. Kwa hivyo, kote kwenye mambo ya maisha maisha kufungwa, kamati imependekeza miaka isiyopungua 30 inaweza kuwa 40, 50, 60 lakini isipungue miaka 30. Kwa hivyo, kifungo cha maisha haikupendelea.

Baadae pia ametoa ushauri mwingi katika mazungumzo yake. Mhe. Mwenyekiti yote hayo tumeyapokea na tunayakubali.

Nikienda kwa Mhe. Rashid Seif Suleiman ,Waziri kivuli wa Wizara hii, yeye ametaka kujua kuhusu hicho choo kipya kilichowekwa *Airport*. Kwa ufupi masuala yake yaliulizwa mengi, kwanza alitaka kujua ni miaka mingapi hivi sasa tokea kuwasili. Ni kwamba ni miaka miwili tokea kuwasili, hicho choo kimeombwa na *DPP*, Mkurugenzi wa Mashtaka wa *UNDP*. Baadae choo hicho kilikabidhiwa polisi ikaamuliwa kifungwe *Airportt*, lakini Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi wakasema kuwa uwanja wakati huo unataka kufanyiwa matengenezo. Lakini sasa sehemu imeshapatikana na ofisi ya Mhe. Waziri Kiongozi itashughulikia kukifunga hicho choo. Choo hicho ni cha aina yake kabisa, kwa hivyo natarajia karibu sana kitafungwa katika Uwanja wa Ndege wa hapa Zanzibar.

Aliuliza pia tume ya zamani imekutana mara ngapi? Jibu ni kwamba imekutana mara moja. Je, kituo cha kutibia wateja kiko vipi au kitapatikana? Mhe. Spika, ni kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tumewasiliana na wadau au washirika wa maendeleo mbali mbali kutaka kusaidiwa katika kufanikisha jambo hili. Juhudi zetu zimeanza kutia sura ya matumaini ambapo Mfuko wa Dharura wa Serikali ya Marekani kupitia *CDC* imeonesha nia ya kufanikisha ujenzi huo wa kituo hapo Tunguu. Kwa hivyo, mshauri wa utengenezaji wa michoro kwa ajili ya kituo hicho yumo katika hatua ya mwisho.

Utafuatiwa na hatua ya utengenezaji wa kitaalamu wa viwango vya vifaa vya ujenzi vinavyohitajika na hatimaye kutangaza *tender* kwa mkandarasi. Kwa hivyo, kuna matumaini kwamba kituo hicho cha tiba kwa walioathirika na madawa, kitajengwa Tunguu ni matumaini yetu. Mpaka sasa hivi tunakwenda vizuri na *CDC*.

Nikija kwa Mhe. Salmin Awadh Salmin yeye alipendekeza kwamba hao wateja wanaosinzia wapimwe na baadae wapelekwe mahkamani. Mhe. Spika, majibu ni kwamba yamepatikana kwenye kamati. Kamati imependekeza kifungu Nam. 19(1) kiongezwe kifungu (c) na kisomeke hivi, "Iwapo atapatikana mtu akiwa anatumia madawa ya *narcotic* na *psychotropic* atapelekwa chuo cha mafunzo kwa muda wa miezi sita na akimaliza atapelekwa kituo cha kurekebisha tabia mpaka atakaporekebishika".

Kwa kifungu hiki Mhe. Spika, kikiwa kwenye sheria hii, basi hao wanaosinzia wote miezi sita ndani, Kamati ndivyo ilivyopendekeza. Sisi hatuna tatizo, kwa hivyo baadae tutaona ile tume itavyokaa nakujadili jambo hili. Kwa sababu hili jambo si dogo walaji unga ni wengi, jela zetu tunazijua vituo vya mafunzo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hapa sitaki kuongeza langu.

Sifa za Mkemia, Mhe. Salmin ametaka kujau sifa za mkemia. Majibu:- Mapendekezo ya Kamati, ukurasa wa 9 kifungu nambari 55 kimetakiwa kisomeke hivi, "Kutakuwa na wakemia wa serikali watakaoteuliwa na waziri wenye taaluma ya kemia, au muhandisi mkemia, au mtaalamu wa biolojia, pamoja na fundi maabara wa kemia, au tiba na mtaalamu wa madawa".

Mhe. Spika, lazima nilifahamishe kidogo, kuna mkemia na kuna Mkemia Mkuu. Mkemia Mkuu wa Serikali huchaguliwa na Mhe. Rais, lakini yule mkemia anayekwenda mahkamani kutoa ushahidi yule ndiye anayechaguliwa na waziri. Kwa sababu inategemea ile kesi ya aina gani pale pa Mkemia Mkuu tunao ma-*chemically engineer*, ma-*process engineer*, ma-*pharmacists*, tunao watu wa aina mbali mbali. Sasa wale ndio wanaitwa wakemia, lakini yule mkubwa wao pale ndiye anayeitwa Mkemia Mkuu. Kwa hivyo, hao wakemia ni nani? Nimekwisha kuwataja.

Halafu ametaka kujua huyu Mkuregenzi Mtendaji ni nani? Mapendekezo ya kamati ukurasa wa 4 kifungu Nam. 4(5) kimetakiwa kuongezwa kifungu kipya cha 2 kinachosomeka, "Mkurugenzi Mtendaji awe na shahada ya sheria na awe na uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitatu', huyu ndiye atakuwa Mkurugenzi Mtendaji na hiyo ndio sifa yake.

Tume ya kitaifa amesema ni kubwa, mawaziri wengi, mapendekezo ya kamati, waheshimiwa wengi wamelizungumza suala hili kwamba, inaonekana tume ya mawaziri wengi, tumezungumza sana kwenye kamati bila ya kiasi. Kwa hivyo, kamati imependekeza kwamba, vifungu Nam. 4(2)(d) , (h) , (i) , (j) , (m) na (n) Vifutwe. Nani watakaofutwa? Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji, Waziri wa Fedha na Uchumi, Mwanasheria Mkuu, Kamishna wa Polisi, Katibu Mkuu Afisi ya Waziri Kiongozi, mtu mwengine yeyote atakayechaguliwa na Waziri Kiongozi na sisi serikali tunapendekeza Mufti pia afutwe. Hayo ndio mapendekezo yetu, kwa hivyo, watafutwa watu saba na tutaifanya tume iliyokuwa ndogo.

Pia Mhe. Salmin Awadh amependekeza kuwa sera ifanyiwe marekebisho. Tumekubali na tutaifanyia marekebisho.

Kuhusu mtu atakaesaidia kutorosha mtuhumiwa. Amesema kifungu hiki hakipo, lakini wataalamu wamesema kifungu hiki kipo, kinasema hivi:-

Ikiwa atakuwa mtu amefanya kosa kwa mara ya kwanza hukumu yake kipo, kifungu Nam. 18, lakini inategemea kosa lipi alilosaidia ambalo amelifanya katika kusaidia, ikiwa kifungu hiki hakikosi basi kuna kifungu chengine Nam. 27 ni adhabu ya kosa ambalo hakuna adhabu iliyowekwa, ikiwa Mhe. Jaji ameona hakuna kosa lakini mtuhumiwa ameingia kwenye kosa, basi atatumia kifungu Nam. 27 kumtia hatiani.

Mhe. Spika, sasa nakwenda kwa Mhe. Aziza Nabahan, yeye amezungumza kwamba ana matatizo ya mtoto wake na sote tumesikitishwa na kitendo hicho. Takriban kila familia katika Zanzibar imeathirika na jambo hili, hakuna asiyeathirika. Ameomba kuwa Mkemia huu unga aliopelekewa *sample* asiite sembe na uitwe kama ulivyo.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii siku moja ilitembelea kwa Mkemia Mkuu wa serikali, mimi nilikuwepo katika ziara ile pamoja na Katibu Mkuu wangu, kuliwa na mjadala mkubwa sana kwa Mkemia Mkuu na ninaomba niwataje waheshimiwa wawili, Mhe. Moh'd Ali Salim na Mhe. Haji Faki Shaali. Waliuliza kwa nini mnaletewa *sample* ya *heroin* au cokein mnasema saruji! Ikawa vuta nikuvute pale. Lakini kamati ya Ustawi wa Jamii Mhe. Spika, safari hii umenipa kamati ya kweli, ni kamati nzuri, inatoa vitu vizuri, inachangia vizuri.

Sasa Mhe. Mwenyekiti wa Baraza hili Mhe. Ali Mzee Ali ni mjumbe wa kamati hii akasema mimi nitasaidia katika kueleza huu ufafanuzi. Mhe. Spika, hapa Zanzibar alikuwepo daktari mmoja jamaa yangu alikuwa akiitwa Dr. Mugheiry, nafikiri Mhe. Burhan Saadat atamjua na baadhi ya waheshimiwa.

Dr. Mugheiry alikwenda mgonjwa mwanamme na jina lake Mhe. Ali Mzee alimtaja kuwa ni Maulid, kwa hivyo, kuna Maulid mwanamme na mwanamke. Sasa yule mgonjwa akasema anaumwa hivi na hivi, basi akasema afanyiwe *test* za kila kitu pamoja na choo kidogo. Akenda maabara kufanyiwa *test* ya choo hicho matokeo yakaletwa kwa Dr. Mugheiry naye akamtizama yule mgonjwa Bw. Maulid kila akimtazama anasema siwezi kusema naona mambo ya maajabu. Akamwambia nieleze, mgonjwa kaomba aelezwe ajue tatizo, akaambiwa tatizo linaonekana humu kwamba wewe ni mjamzito.

Hii Mhe. Spika, nimemuomba Mhe. Ali Mzee aniruhusu ili niliseme na amenipa ridhaa yake ndio maana ninalizungumza. Yule mgonjwa akasema anataka kujua nani aliyemtia mamba ile, basi pakafanywa uchunguzi pale, nyumbani kuna mama yeyote? Akasema niko peke yangu, umeutia saa ngapi? Nimeutia sasa hivi asubuhi na nikauleta, akaambiwa ndio mjamzito. Ukafanywa uchunguzi pale, kumbe *orderly* aliyechukua ile *sample* ya mkojo amekwenda kwenye ngazi amejikwaa ule mkojo ukamwagika akaingia chooni akautia wake yeye akaupeleka maabara.

Mhe. Spika, ama pale kwa mkemia suala hili pale pale lilimalizika, limemalizika kwamba kinachopelekwa ndicho kinachotolewa *result*, wakipelekewa saruji watasema saruji, sasa hawajapelekewa *cocaine* watasema nini. Mhe. Spika, niendelee.

Lakini sheria hii mpya imeliona hilo na imeweka kanuni kifungu Nam. 70 (2)(f) inayosema, 'kutolewa kwa *sample* na majaribio na uchambuzi wa *sample* hiyo'. Katika kamati tumeelezwa na wataalamu kwamba safari hii ukishakukamatwa ule mzigo basi unakuwa *sealed*, unakuwa *signed* na huwezi kuufungua, utafunguliwa mbele ya Mkemia. Ukishafunguliwa ule mzigo Mkemia mwenyewe atatoa *sample* anayoitaka kiasi kidogo akishakutoa mzigo ule unafungwa tena unakuwa *sealed*. Kwa hivyo, yeye atakuwa vitu alivyovitoa mbele ya mashahidi na wata-*sign* wote waliokuwepo na watahakikisha jambo hilo. Ile *sample* itakwenda ofisini kwake itachunguzwa na sio tena ile polisi itoe mzigo imwambie chunguza, hapana.

Umewekwa utaratibu maalum na kanuni ya kifungu hicho imeipa uwezo tume, ikiona kama mambo hayendi vizuri basi itaunda kanuni nyengine au kanuni, itatoa namna gani sample itaweza kuchukuliwa na kuchambuliwa au uchambuzi wa *sample.* Kwa hivyo, nafikiri sheria hii kila kitu kimezingatiwa. Michango yote aliyotoa Mhe. Aziza Nabahan tumeipokea na yote tutayafanyia kazi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira kaeleza vizuri sana na tunamshukuru kwa michango yake na ufasaha wake alioueleza.

Mhe. Ali Denge Makame alipenda kuwa adhabu iwe kali ili suala hili lipungue la madawa ya kulevya. Tunakubaliana naye Mheshimiwa, kwa hivyo, mswada huu umeliona hilo.

Pia amependekeza ufanywe upekuzi wa ghafla asingojewe shahidi. Mswada huu umeliangalia hilo na ipo katika kifungu cha 32, 33 na 34. Sasa Mhe. Spika, katika sheria hii mswada huu unaruhusu *ambush*, askari watavamia, watavunja wataingia, sio sasa hivi mpaka umtafute sheha, shahidi wa tatu hata ukigonga mlango dawa zishapigwa *flush* ishakwenda chooni, lakini sasa hivi sheria hii imeliona itapigwa *ambush* na kutavunjwa watu watavamia kila kitu kimeangaliwa mambo yote yamewekwa sawa. Ukiusoma huu waraka wa mswada vizuri na ukiangalia yale mapendekezo ya kamati basi mswada huu takriban ni mzuri matarajio yetu.

Pia amependekeza hukumu ya kifo au maisha. Tumeliona hilo lakini tumeweka isiopungua miaka 30 na kuendelea. Kwa hivyo, hilo limeangaliwa na tunamshukuru sana Mheshimiwa kwa kazi nzuri ya mchango wake aliyoifanya.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk mchango wake ni mzuri na tumeupokea. Kuhusu kuwa iwepo *line* ya simu kutoa taarifa, wazo lake ni zuri na tutalichukua litafanyiwa kazi. Pia ametaka mkemia awajibike vizuri, hakuna tatizo tutalifanyia kazi suala hilo.

Kwa ujumla mchango wa Mhe. Makame Mshimba ulikuwa mzuri, alitoa mifano mbali mbali ya kuonesha kwamba kuna baadhi ya watu sio waaminifu na wengine wanajigamba kwamba wao wana uwezo katika jambo hili. Lakini sheria hii itamkamata yeyote atakayeweza kujionesha kwamba yeye ana uwezo, ni matumaini yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi alisema kwamba sheria hii ifanye kazi, ni matarajio yetu. Pia ametaka kujua kwamba wako waliorejea hali zao za kawaida baada ya kutumia hii dawa? Mhe. Spika, wapo na yupo kijana mmoja nimeambiwa hivi sasa amerudi *South Africa* na amekwenda mara mbili *America*. Yeye ameamua kuacha madawa, sasa hivi ni kijana mzuri na katika ujumbe unaokwenda Marekani, Michigan pamoja na Mkurugenzi wetu wa madawa ya kulevya yeye alikuwemo, nimeambiwa amekwenda mara mbili Marekani, na yeye sasa hivi anatumika kama ni mwalimu wa kutoa elimu ili na wengine waache mambo hayo. Kwa hivyo, wapo na tunao kwenye kitengo chetu cha madawa ya kulevya.

Pia alipendekeza kwamba Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi awemo kwenye tume kwa sababu bandari na *airport* anashughulikia. Ni kwamba tumeliona hilo, isipokuwa tumechukua kuwa Mkuu wa *Custom* au Msimamizi Mkuu wa mambo ya *custom* ya A*irport* na bandari yeye tumempendekeza awe katika sekretarieti. Kwa hivyo, amewekwa mtu wa mambo ya bandari.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na yeye ametoa mchango wake mzuri sana tumeuchukua, amezungumza vizuri mambo ya mbwa. Mbwa *airport* alikuwepo lakini mbwa yule amefariki. Kwa hivyo, tuna mpango wa kutafuta mbwa mwengine tumuweke.

Mhe. Ame Mati Wadi wa Jimbo la Matemwe yeye ni mjumbe wa kamati na makamo mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Ni kwamba michango yake ni mizuri na takriban yote aliyochangia tulikuwa pamoja kwenye kamati na anaufahamu sana mswada huu wa sheria. Amependekeza kwamba zawadi iwekwe kwenye mswada huu. Zawadi imo na itakuwa inatolewa kwa vizuri sana kwa wote ambao watastahiki kupewa zawadi, tume ndio moja ya kazi yake katika mambo hayo. Kwa hivyo, Mheshimiwa na wewe tunakushukuru sana kwa michango yote uliyoitoa.

Halafu Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi michango yake ni mizuri kabisa na takriban yote tumeipokea. Isipokuwa alitaka kujua tu kwamba, kwa njia ya kuwaadhibu wakosa, vipi kuhusu mambo ya fedha? Tunaona fedha pia inastahiki kuwemo katika sehemu ya adhabu, kwa sababu hapa fedha tunaweka ni kama adhabu kwa yule mtu aliyefanya kosa.

Nikija kwa Mhe. Ali Abdalla Ali yeye alikuwa anataka ufafanuzi neno ‘uchukuzi’ amesema viko vyombo vyengine mbali mbali vinavyochukua hivyo ametaka neno hili lifanyiwe marekebisho lisemwe kuwa vyombo vyengine vinavyochukua vitu mbali mbali yaongezwe. Tumekubaliana naye hakuna tatizo. Kwa hivyo, neno hili la uchukuzi lizomeke vizuri.

Neno ‘ufukiaji’ alisema litumike neno ‘kupanda’. Tumezungumza na wataalamu wameona kweli Kiswahili sahihi hapa ni kupanda sio ufukiaji. Halafu mambo ya mchakato ameliona neno ‘mkasumba’ maana yake unaotengenezwa kwa matumizi ya dawa badala ya kutumia neno ‘mchakato’, pia wamekubali wataalamu wangu. Neno ‘kuuza’ amesema ni kutangaza au kuweka bayana. Kwahivyo, pia limeonekana ni neno sahihi. Mirungi wataalamu wamesoma wamesema mirungi ni mimea au miraa inayotumika kutafunwa ikiwa mibichi na huleta nishai. Kwa hivyo, hiyo ndio *definition* ya mirungi.

Kifungu Nam. 4 amesema tume ni kubwa ya watu 14 wote wote jumla 26. Sasa tume tumeshaipunguza kwa mujibu wa mapendekezo ya kamati na sekretarieti, pia imepunguzwa tutakuja kuiona huko baadae. Kwa hivyo, wote wamepunguzwa na kamati imeto mapendekezo mazuri sana, ukiangalia mapendekezo ya kamati yote tumeyaafiki na tunakubaliana nayo.

Halafu akasema kazi ya tume ni kuboresha na kusimamia, hivyo kazi ya kusimamia ipo katika kifungu Nam. 7(1)(f). Hilo tumeliona na linajieleza katika kifungu Nam. 7(1)(f).

Vile vile chanzo cha mapato amesema kwamba kazi ya tume ni kusimamia matumizi na kukusanya, yeye neno kukusanya haliwafiki, lakini jibu tume itasimamia na sio kukusanya ilivyokusudiwa kwenye mswada huu. Kwa hivyo, nakubaliana nayeye.

Halafu amesema ripoti ya tume kwamba, inaonekana kuwa mara mbili italetwa kwenye Baraza ,yeye amependekeza iwe mara moja, ni sawa kabisa, kifungu cha 8 na kifungu cha 12(4) vyote vinaeleza ripoti kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, tunawafikiana na yeye kwamba iwepo ripoti moja ya kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi, hivyo kifungu cha 8 na kifungu cha 12(4) kinaungana pamoja Mhe. Spika.

Kuhusu adhabu yeye ametaka iwepo adhabu moja tu, ukikutwa na kitu kidogo au kikubwa cha dawa za kulevya. Suala hili haiwezekani, kwa hivyo, ni vizuri iachiwe Mahkama itoe adhabu kwa kuona wingi na kidogo wa dawa zenyewe. Yeye ametaka ukionekana dawa kidogo,au ukionekana na dawa nyingi, yote upigwe hukumu moja tu, lakini wataalamu wanasema suala hili haiwezekani, ni vizuri iachiwe mahkama itoe adhabu kwa namna inavyoona wingi na kidogo.

Kifungu nambari 21 adhabu kwa ubadhirifu kwa mkulima aliyeidhinishwa. Kifungu hiki kimefutwa, mambo yote ya kulima hapa nchini kwa mujibu wa kamati tulivyozungumza vyote vimefutwa kufuatilia mapendekezo ya kamati ukurasa wa tano. Kwa hivyo, kamati imependekeza hakuna ruhusa tena ya kulima aina zote za dawa za kulevya hapa Zanzibar. Kwa hivyo, kama kuagizia tufuate utaratibu wa kuagizia kwa matumizi ya mwanadamu lakini sio kulima. Kwa sababu kamati imesema ukianzisha ruhusa ya kulima ndio unaacha njia za watu kuchukua hivyo vitu.

Sasa niende kwa Mhe. Zakiya Omar Juma suala la mbwa aliyekufa. Je, mbwa huyu amekufa kwa sababu gani? Mbwa huyu nimeambiwa amefariki kwa homa ya mapafu, lakini hivi sasa tunafanya mipango ili aletwe mbwa mwengine kama Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi alivyopendekeza.

Pia amependekeza sheria hii iwe kifungo cha maisha. Kamati imeliona hilo na imesema ni vizuri tuseme isiyopungua miaka 30. Kwa hivyo, kama mtu kule anakwenda miaka 40 anapigwa na miaka 30 yake inakuwa 70 ndio maisha hiyo. Mhe. Spika, pia tunamshukuru Mhe. Zakiya Omar Juma kwa yote aliyoyaeleza.

Mhe. Ashura Abeid Faraji aliuliza je, madawa yamewahi kuangamizwa. Mhe. Spika, mwaka jana yaliangamizwa Mahonda, Kiwanda cha Sukari. Kifungu cha 56 kinaeleza wazi wazi namna gani kuangamiza madawa hayo yanayokamatwa. Pia tunampongeza Mhe. mwakilishi kwa mchango wake mzuri.

Sasa nakwenda kwa Mhe. Hija Hassan Hija. Mhe. Spika, Mhe. mwakilishi amependekeza suala la tume kuwa na mawaziri wengi, amependekeza maofisa au watendaji wawe wajumbe wa tume na sio mawaziri. Jibu Mhe. Spika, tume itakuwa inasimamia, kufafanua, kukuza na kuratibu sera ya serikali kuhusu biashara haramu ya dawa za kulevya. Kwa hivyo, tumeona kazi ya tume ni kusimamia, kufafanua, kukuza na kuratibu serikali ya serikali kuhusu biashara haramu ya dawa za kulevya. Sasa tumeona mawaziri ndio wana wajibu wa kuisimamia hiyo sera.

Lakini wataalamu na watendaji watakuwa wajumbe wa sekretarieti. Tafadhali angalia ukurasa wa 4 mapendekezo ya kamati kuhusu sekretarieti. Kwanza atakuwa Mkurugenzi mtendaji ndio Mwenyekiti. Pili mjumbe kutoka Kitengo cha Polisi cha Madawa ya Kulevya. Tatu mjumbe kutoka Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka *(DPP).* Nne mjumbe kutoka kwa Mwanasheria Mkuu. Halafu mjumbe kutoka *Custom Prevention Services.* Halafu mjumbe kutoka Afisi ya Mkemia Mkuu. Mjumbe kutoka Mwanasheria wizara husika. Mjumbe kutoka mtakwimu Mkuu wa Serikali na Uratibu wa Madawa ya Kulevya.

Utakuta hawa ndio wataalam, ndio wanaounda sekretarieti. Kwa hivyo, hawa ndio watakuwa na jukumu kupeleka na kuandaa kila kitu kwenye tume. Tume itakuwa zaidi juu ya sera.

Mswada huu umezingatia kupata mapato kwa njia ya kufilisi mali. Jibu, zipo fedha zitakazotolewa na serikali kifungu cha 9 (2) © kama ruzuku na michango tu. Kwa hivyo, suala la kwamba tume inategemea zaidi mambo ya kufilisi mali sio sahihi kwa sababu bado kiko kifungu cha 9 (2) © kinachosema kwamba michango ya serikali itakuwepo.

Ametaka kujua Mkemia Mkuu. Mkemia Mkuu ni kweli alikuwa Mkemia Mkuu amefariki dunia na hivi sasa tumo katika mchakato wa kupata Mkemia Mkuu

mwengine na aliyekuwepo sasa hivi ni Mfamasia ambaye anakaimu nafasi hiyo na anafanyakazi vizuri. Kuhusu stahili zake tutampatia.

Masaa mangapi ya uchunguzi ifanywe ili ukweli upatikane badala ya haraka tu. Mhe. Spika, ni kwamba hili tumeliona kwenye kamati na tunamshukuru Mhe. Mwakilishi ameliona hili. Kamati tumekubaliana kwamba baina ya masaa 24 na yasiyozidi 48 sampuli iwe imeshapelekwa kwa kutambuliwa. Kwa sababu wakati mwengine mteja atakayekuja uwanja wa ndege itatakiwa akae pale masaa mpaka zile pipi zimalizike kutoka. Kwa hivyo, tumehofia kuweka masaa kamili. Tumechukulia tu pipi zinaweza kumalizika mpaka masaa 48, lakini kipindi hicho inatakiwa sampuli iwe imeshachukuliwa na imeshapelekwa kule kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kwa uchunguzi. Kifungu chake kiko namba 47 ya masawazisho.

Mhe. Spika, sasa tunakwenda kwa Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim. Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi kazungumza mambo mengi, mifano mbali mbali na kwa kweli yote hayo tumeyakubali na tumeyachukua. Amependekeza kuwepo na ushauri wa Kamati za Shehia, Kamati za Wilaya, Mkoa, Taifa. Mswada huu umezingatia hilo na kupewa jukumu tume kuunda Kamati za Ufundi. Kwa hivyo Mhe. Spika, yote uliyoyazungumza tumeyachukua, tunayapokea na mifano mbali mbali.

Kuhusu ukulima kutolewa ruhusa kifungu cha 15 na 16 vyote vimefutwa na mapendekezo ya kamati. Kwa hivyo, hakuna ruhusa ya kulima Zanzibar shughuli yoyote ikiwa pendekezo hili litakubalika. Hili pia limechangiwa na Mhe. Zahra Ali Hamad kwa maandishi.

Mhe. Spika, kudhibiti kwa madawa ya matumizi ya binadamu hospitali Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim alitaka kujua. Vipi matumizi ya dawa hizi kwa binadamu hospitali. Mhe. Spika, mswada huu pia umezingatia suala hilo. Kwa hivyo, hakutokuwepo na uvujaji wa madawa, atakayevujisha sheria itamkamata na itamhukumu na kifungo chake kimo na faini zake zimo zote zimeainishwa. Mhe. Spika, takriban mswada huu umezingatia kila kitu.

Mhe. Ali Moh'd Bakari yeye ametaka watuhumiwa wasipewe dhamana. Mhe. Spika, mswada huu umezingatia, ukisoma vizuri utakuta yako makosa hayana dhamana. Amependekeza maelewano ya pamoja katika kupiga vita madawa ya kulevya, hilo ni jambo muhimu sana na mambo yote aliyochangia Mhe. Mwakilishi tumeyasikia, tumeyapokea.

Mhe. Spika, Waheshimiwa wamezungumza mambo mengi yote tumeyachukua tutayafanyia kazi, ya kurekebisha ndio tumeyarekebisha na mengine

nimeyaruka ruka pengine yamenipita. Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima ili kupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya na Kuweka Masharti ya Uzuiaji Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Nakotiki na Aina za Saikotropiki

KAMATI YA BARAZA ZIMA

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Kifungu 1	Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 2	Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake.

SEHEMU YA PILI

Kuanzishwa kwa Tume ya Mawaziri ya Kuratibu Udhibiti wa Madawa ya Kulevya Pamoja na Marekebisho yake

Kifungu 3	Jukumu la Serikali kuchunguza hatua za uzuiaji matumizi mabaya ya madawa ya kulevya pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 4	Kuanzishwa kwa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Madawa ya Kulevya pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 5	Mikutano ya Tume pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 6	Mjumbe mualikwa.
Kifungu 7	Kazi za Tume na Sekretarieti.

Kifungu 8 Ripoti ya Tume kuwasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi.
Kifungu 9 Bajeti ya Tume pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 10 Mkurugenzi Mtendaji kuandaa makubaliano.
Kifungu 11 Tume kusimamia fedha kwa mahitaji mengineyo pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Tatu

Mfuko wa Udhibiti wa Matumizi mabaya ya Madawa ya Kulevya

Kifungu 12 Kuanzishwa kwa Mfuko na marekebisho yake.

Sehemu ya Nne

Marufuku Kupatikana na Madawa ya Kulevya na Kufanya Biashara ya Madawa ya Kulevya Pamoja na Upandaji wa Baadhi ya Miti Pamoja na Marekebisho yake

Kifungu 13 Marufuku kulima baadhi ya mimea.
Kifungu 14 Kutengeneza Madawa ya Nakotiki na Saikotropiki pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 15 uwezo wa Tume kuruhusu Udhibiti na Usimamiaji Ukulima, uzalishaji, uuzaji wa kasumba, majani ya kasumba na mirungi kimefutwa.
Kifungu 16 Madawa ya Nakotiki na Saikotropiki kuhusika kushikiliwa kimefutwa.
Kifungu 17 Vikwazo katika kushughulikia na madawa aina ya Nakotiki na Saikotropiki kinafutwa.

Sehemu ya Tano

Makosa na Adhabu

Kifungu 18 Adhabu kwa kupatikana na/au kununua madawa ya koka au nakotiki pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 19 Adhabu kuhusiana na kupatikana na kiasi kidogo cha madawa ya Nakotiki na Saikotropiki pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 20 Adhabu kuhusiana na kutoa madawa ya kulevya aina ya Nakotiki na Saikotropiki.

Kifungu 21 Adhabu kwa ubadhirifu wa mkulima a liyeidhinishwa kimefutwa.
Kifungu 22 Adhabu kwa kukiuka masharti, leseni au ruhusa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 23 Adhabu kwa kugharimia shughuli haramu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 24 Adhabu kwa kusaidia kufanya kosa chini ya sheria hii pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 25 Kujiandaa au kujaribu kufanya kosa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 26 Adhabu kwa kutenda baadhi ya kutiwa hatiani kwa kosa la awali pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 27 Adhabu kwa kosa ambalo hakuna adhabu iliyowekwa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 28 Dhana kuhusiana na uwezo wa kiakili.
Kifungu 29 Makosa yasiyo dhamana pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 30 Makosa ya Makampuni.
Kifungu 31 Utoaji wa baadhi ya wateja kwa ajili ya matibabu kimefutwa.
Kifungu 32 Uvamizi wa kuingiza wakati wa dharura pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 33 Upekuzi na kukamata bila ya waranti wakati wa dharura pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 34 Mamlaka kutumia njia muafaka ya kivuli.
Kifungu 35 Mamlaka kutumia mali inayotolewa chini ya udhibiti, mitego au operesheni ya siri pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 36 Zawadi.
Kifungu 37 Kuwalinda watoa habari pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Sita

Taratibu

Kifungu 38 Kutumiwa kwa Sheria ya Mwenendo wa Jinai pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 39 Utaratibu wa kukamata pale ambapo kufilisi haiwezekani kimefutwa.
Kifungu 40 Wajibu wa wamiliki wa ardhi kutoa taarifa za ukulima usio halali wa mazao kimefutwa.

Kifungu 41	Uwezo wa kukamata mazao yaliyolimwa isivyo halali.
Kifungu 42	Tume kuelekeza uangamizwaji wa vitu kadhaa pamoja na marekebisho yake.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hapa kuna marekebisho ya *marginal note, marginal note* iliyopo imerekebishwa na hiyo iliyosomwa sasa ndio sahihi.

Kifungu 43	Kuhusika kwa maelezo katika mazingira maalum.
Kifungu 44	Dhana ya kupatikana vitu visivyo halali pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 45	Maafisa walioidhinisha kuchukua dhamana ya vitu vilivyokamatwa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 46	Jukumu la Maafisa mbali mbali kusaidiana pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 47	Vitu vilivyokamatwa na kushikiliwa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 48	Adhabu kwa kutoa maelezo ya uongo.
Kifungu 49	Adhabu dhidi ya afisa kukataa kutekeleza wajibu wake au anayemsaidia wakosaji pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 50	Uwezo wa kufilisi bidhaa au vitu, n.k kuhusiana na kosa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 51	Kufilisi iwapo hakuna hatia pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 52	Dhana kuhusiana na nyaraka katika masuala kadhaa.
Kifungu 53	Uwezo wa afisa aliyeidhinishwa kuitisha maelezo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 54	Utaratibu kuhusiana na uchambuzi wa madawa yaliyokamatwa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 55	Uteuzi wa Mkemia wa Serikali pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 56	Uangamizaji madawa yaliyokamatwa pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Saba

Kutaifishwa kwa Mali iliyopatikana Kutokana na/au Iliyotumika Katika Biashara Haramu ya Madawa

Kifungu 57	Kutaifishwa mali pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 58	Kukatazwa kumiliki mali iliyopatikana kinyume na sheria pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 59	Mahakama kuruhusu upelelezi au ukaguzi.
Kifungu 60	Jukumu la kuthibitisha.
Kifungu 61	Malipo mbadala pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 62	Rufaa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 63	Uwezo wa kuchukua miliki pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 64	Mipango kuhusiana na alama, kujulisha n.k kwa mali.

Sehemu ya Nane

Masharti Mengineyo

Kifungu 65	Kinga kwa hatua iliyochukuliwa kwa nia nzuri pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 66	Tume kuzingatia mikataba ya kimataifa wakati ikiweka kanuni pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 67	Uwezo wa serikali kuanzisha vituo vya kutambua tiba n.k kwa wateja na kwa kusambaza madawa ya nakotiki.
Kifungu 68	Uwezo wa Tume kutoa muongozo.
Kifungu 69	Uwezo wa kukasimu madaraka pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 70	Uwezo wa Tume kuweka kanuni.
Kifungu 71	Kutumika kwa Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Umoja wa Afrika Mashariki ya 2004.
Kifungu 72	Uwezo wa kuondoa shaka.
Kifungu 73	Kufutwa kwa Sheria Nam. 16 ya 2003.
Kifungu 74	Kubakiza na masharti ya mpito.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kuna vifungu vimefutwa, sasa mtiririko wa vifungu hivi mpaka kufikia mwisho vitakuja kupungua baadae haitakwenda kama hivi tulivyoisoma, vitapungua kutokana na vile ambavyo tumekubali kuvifuta.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu baada ya kifungu na kuukubali bila ya mabadiliko yoyote pamoja na masahihisho, sasa naliomba Baraza lako tukufu likubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubali mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya ya 2009

(Kusomwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya ya 2009 usomwe mara ya pili. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji waheshimiwa wajumbe wale wanaokubali mswada huu pamoja na marekebisho yake katika kusomwa mara ya pili wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya pili na kupitishwa)

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nadhani kama mlivyoona Katibu hakuisoma vizuri kwa hivyo labda kuna haja ya kusomwa vizuri.

Mhe. Spika: Nashukuru Mhe. Haji Faki Shaali, hata Rais Barack Obama aliapishwa mara mbili, kulitokea makosa ya aina kama hii kwa hiyo ikaonekana lazima yasahihishwe vyenginevyo asingekuwa Rais rasmi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa kuwa waheshimiwa wajumbe wamemaliza kazi ngumu ya kupitisha miswada na tumemaliza kabla ya wakati, naomba kutoa hoja kwamba uliahirishe Baraza lako tukufu mpaka siku ya Jumatatu tarehe 26/10/2009 saa 3:00 asubuhi. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Mawasilianao na Uchukuzi: Mhe. Spika naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa kazi nzuri mliyokwishaimaliza. Kesho semina ipo nafikiri tumeshaarifiwa, *registration* itaanza saa 3:00 asubuhi hapa hapa Ukumbini. Lakini kutokana na kazi nzuri basi tuliyoifanya, nachukua nafasi hii kuahirisha kikao hiki mpaka siku ya Jumatatu tarehe 26/10/2009 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 12:00 jioni Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 26/10/2009 saa 3:00 asubuhi)